30007

# IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA,

# CHUO KIKUU CHA KENYATTA.

# MTAZAMO MPYA WA USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA UTENDI WA MAISHA YA ADAMU NA HAWAA NA PARADISE LOST

NA:

MULI DAVID KIAMBA

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

2011

Kiamba,Muli David
Mtazamo mpya wa usawiri wa mwanamke
2011/359842

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine.

.................................... ..........................................

**MULI D. KIAMBA** **Tarehe**

**C50/CE/15542/05**(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika chuo cha Kenyatta

.................................... ..........................................

**DKt. E. Masinde** **Tarehe**

.................................... ..........................................

**Dkt C. Momanyi** **Tarehe**

## TABARUKU

**Kwa**

Mke wangu mpenzi, Agnes N. Kasyoka, na wanawake wote wanaodumisha ndoa zao na kupigania haki zao...

**Kwa**

Watoto wangu wapenzi, Mwende, Mutinda, Mumbua, Muli na Kasyoka ...

Sina kingine zaidi cha kuwarithisha.

## SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kunipa uhai na uwezo wa kuvuka visiki vingi vya kiakademia hadi kiwango hiki cha uzamili... Na hesabu baraka moja moja tu, nami naona ni ajabu kuu ...

Napenda kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. C. Momanyi na Dkt. E. Masinde kwa ushauri, subira, na shinikizo mwafaka vilivyonipa ghera ya kumaliza kazi hii.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika kwa kunikanda kiakademia ...Athari za mwalimu bora hubaki kovu la faraja kwa mwanafunzi. Wema hauozi, na hulipwa papa hapa duniani.

Wazamili wenzangu, Njeru Mbogo, Rajwayi Caleb, Regina Wathome, Roda Mogaka na Jane Maithya... Tulifaana kwa mengi kuliabiri jahazi hili la elimu hadi ufuoni. Ahsanteni kwa kunifaa kwenu.

Shukrani za jazila ni kwa aila yangu - mke na wanangu: Mlivumilia mengi kipindi hiki chote, mlinipa utulivu wa moyo. *Wanangu, elimu ni ukwasi.*

## YALIYOMO

Mada .......... (i)

Ikirari .......... (ii)

Tabaruku .......... (iii)

Shukrani .......... (iv)

Yaliyomo .......... (v)

Vifupisho na Istilahi muhimu zilizotumika .......... (viii)

## SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1 Udurusu wa maandishi .......... 3

1.2 Suala la utafiti .......... 7

1.3 Nadharia tete .......... 8

1.4 Madhumuni ya utafiti .......... 9

1.5 Sababu za kuchagua mada .......... 9

1.6 Upeo na mipaka .......... 11

1.7 Msingi wa nadharia .......... 12

1.7.0 Utangulizii .......... 12

1.7.1 Nadharia ya Udenguzi .......... 13

1.7.2 Nadharia ya Ufeministi .......... 14

1.7.3 Mihimili changamano-Unisai wa Kidenguzi .......... 23

1.8 Mbinu za utafiti........................................................................ 23

1.8.1 Uchanganuzi na uwasilishaji wa data................................. 24

## SURA YA PILI

2.0 Historia ya John Milton ................................................................ 25

2.1.1 Utangulizi ........................................................................ 25

2.1.2 Ukoo na elimu.................................................................... 26

2.1.3 Matukio ya kihistoria na kisiasa ............................................ 29

2.1.4 Upofu wa Milton ................................................................ 33

2.1.5 Maisha ya ndoa ................................................................ 36

2.1.6 Baba na binti zake ............................................................ 38

2.1.7 Athari za ndoa katika uandishi wa P.L ................................. 40

2.2.0 Historia ya Abdilatif Abdalla .................................................. 42

2.2.1 Utangulizi ........................................................................ 42

2.2.2 Maisha ya Abdilatif Abdalla .................................................. 42

2.3.0 Uwiano na utofauti wa waandishi hawa,........................ 45

## SURA YA TATU

3.0. Uchanganuzi wa Utendi wa Adamu na Hawaa na Paradise Lost :

- Misingi ya Unisai wa kidenguzi .............................................. 48

3.1.0 Utangulizi ................................................................ 48

3.1.1 Uchanganuzi wa Utendi wa Adamu na Hawaa............................ 49

3.1.2Kijalizo........................................................................................ 64

3.2. Muhtasari wa Paradise Lost .......................................................... 67

3.2.0 Utangulizi .......................................................................................... 67

3.2.1 Uchanganuzi wa Paradise Lost .................................................... 68

3.2.2 Kiishilio ................................................................................................ 79

## SURA YA NNE

4.0 Mtazamo mpya wa usawiri wa mwanamke .................................. 87

4.1 Utangulizi .............................................................................................. 87

4.2 Mwanamke kama mwenye hekima ............................................... 88

4.3 Mwanamke kama mwenye nguvu ................................................. 92

4.4 Mwanamke kama mwamuzi wa maswala muhimu maishani ......... 100

4.5 Mwanamke kama mtoaji wa majina ............................................ 108

4.6 Mwanamke kama shujaa ................................................................ 114

4.7 Mwanamke kama mpatanishi ......................................................... 121

4.8 Kiishilio .............................................................................................. 123

## SURA YA TANO

5.0 Utangulizi .......................................................................................... 126

5.1 Mahitimisho ...................................................................................... 126

5.2 Hitimisho na matokeo ya utafiti ................................................... 127

5.3 Mapendekezo ..................................................................................... 130

MAREJELEO ............................................................................................ 131

## VIFUPISHO

**P.L**...... Paradise Lost

**T.M**.... Tafsiri ya Mtafiti

**MH**... Mhariri

**FIDA** ....Shirika la mawakili wa wanawake linalotetea haki za wanawake.

## ISTILAHI MUHIMU

### Mfumo wa kuumeni / Ubabedume

Mfuno wa kijamii unoamtukuza mwanamume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke-Humfanya mwanamume msingi mkuu na kaida kuu ya kijamii.

Mfumo huu huzichukua amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatwa katika Jamii nzima.

### Ufeministi

Hujumuisha mikabala mbalimbali ya kuhakiki ambayo, kwa pamoja, licha ya kuwa tofauti, inaelekea kukubalika au kuafikiana kwenye masuala kadha na malengo yake ya kimsingi-Hutumiwa kurejelea Juhudi za kupigania ukombozi wa wanawake kutokana na pingu za kiutamaduni, kidini, kijamii,kisiasa,na kiuchumi- Huitwa pia unisai.

**Wingine**

Dhana hii inatumiwa sana katika uhakiki wa kifasihi wa siku hizi.Kumwelezea mtu,Asasi au kundi fulani kama Wingine ni kumbagua mtu huyo, kuibagua asasi au kundi hilo na mfumo wa kikaida au mkuu katika jamii.

Wafuasi wa nadharia ya Ufeministi wanaamini kuwa mfumo wa Kiubabedume unaishia kuwaangalia wanawake kama Wingine.

**Udenguzi**

Hii ina maana sawa na udhahania.Hueleza hali ambapo kinacholengwa hakiwezi kuhusishwa moja kwa moja na uhalisia au urejelezi unaofahamika.Msingi mkuu ni uwazaji au mawazo ya akili bali sio kitu kinachoweza kuguswa au kuonekana. Udenguzi huliona jambo kwa namna nyingine,na si ile iliyozoeleka.

# SURA YA KWANZA

## 1.0. UTANGULIZI

Kuna utafiti mwingi uliofanywa juu ya mwanamke. Baadhi ya maulama wamechunguza taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika tamthilia, riwaya na hali kadhalika wengine katika ushairi andishi na ushairi – simulizi. Katika ushairi andishi, watafiti wamejikita katika methali, nyimbo na bahari mbalimbali za ushairi kama vile tenzi, mashairi na kadhalika. Chacha (1980) alifanya uchunguzi juu ya ushairi wa Abdilatif Abdalla. Hapa alichambua kazi zake mbili ,yaanii *Utendi wa Maisha ya Adamu* na *Hawaa* na *Sauti ya dhiki.* Momanyi (1991, 1998) alishughulikia matumizi ya taswira kama kielelezo cha uhalisi katika utenzi wa Al-Inkishafi. Kadhalika alifanya utafiti juu ya *Utenzi wa Mwana Kupona*, mashairi ya Munyaka Bin Haji, na S.Robert, huku akiangalia picha ya mwanamke katika jamii ya Waswahili Waislamu.

Masinde (1992, 2003) alitafiti juu ya mashairi na kuangazia uchambuzi wa dhamira na mtindo. Alibobea zaidi na kuangalia ushairi wa Kiswahili – Maendeleo na mabadiliko ya Maudhui.

Karama (1996) alijikita katika Al-Inkishafi na kutafitia ushahidi wa usemezo katika ushairi wa Kiswahili.

Nyanchama (2004) aliegemea katika matumizi ya taswira na ishara katika *Sauti ya Dhiki*.

Matokeo ya tafiti zinazohusu mwanamke yana umuhimu kwani yanatoa nafasi ya mwanamke katika maisha. Baadhi ya kazi zinaonyesha jinsi mwanamke anavyojaribu kujiboresha ilhali zingine zinaonyesha anavyodunishwa.

Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi nyingi za fasihi ni hasi, kuanzia tungo za zamani kama vile *Utendi wa Mwanakupona*, ingawa sasa tufani ya mabadiliko imepiga kasi. Tatizo kubwa linalouathiri usawiri wa kike na jamii nzima ya kike inayopatikana katika fasihi ya Kiswahili linaonyesha hisia za mwamko au mzinduko ambazo zinafifia baada ya muda au waandishi wanaamua kutoziendeleza. Picha hizi za ndivyo sivyo zinaakisi mtazamo mzima wa jamii kuwahusu wanawake.

Mwanamke ni mlaumiwa wa maovu yote ya kijamii, hasa katika mfumo wa ubabedume, hivyo uhuru wa mwanamke unaonekana kuwa kinaya. Ili kumwelewa mwanamke vizuri zaidi, mtafiti amehakiki picha ya mwanamke katika *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* (Abdilatif Abdala) na *Paradise Lost* (John Milton). Tendi hizi zinamwangazia Hawaa, (mwanamke wa kwanza)kama ruwaza ama dhana ghadi ya wanawake wote. Utafiti huu ulilinganisha picha ya mwanamke kwa mwelekeo chanya.

## 1.1 UDURUSU WA MAANDISHI

Usawiri wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili umeshungulikiwa na watu wengi. Ibura ni kwamba wengi wamemsawiri mwanamke kama kiumbe duni, anayedhulumiwa na asasi za dini, utamaduni na ndoa. Usawiri huu umefanywa katika fasihi simulizi na fasihi andishi.

Matteru (1982) ameaua taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Tanzania. Katika utafiti wake, anasema kuwa mwanamke amesawiriwa kama mama, chombo cha kumfurahisha mwanamume na ni mali ya mwanamume. Utafiti huo haukuwa linganishi wala haukujikita katika msingi wa dini yoyote, hivyo ni tofauti na huu.

Muindi (1990) ameangalia usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya S.A. Mohamed. Alijadili sababu zinazowaingiza wahusika hawa katika ukahaba na namna wanavyojaribu kujiondoa kutoka katika maisha hayo.Mtafiti aliangalia usawiri mpya wa mwanamke kwa njia chanya, huku akirejelea Biblia na Korani.

Mule (1991) alichunguza suala la mwanamke katika tamthilia ya Kiswahili kwa kurejelea kazi zilizoandikwa na waandishi wa kike. Utafiti huu umejikita katika

tenzi, haswa zilizoathiriwa na maono ya kidini - Kiislamu na Kikristo- ili kumsawiri mwanamke upya.

Mekacha (1993) katika 'Mwanamke ni Ibilisi' aliangazia picha ya mwanamke katika nyimbo za siku hizi. Anasema kuwa mwanamke amesawiriwa kama mchapakazi, mwenye busara na mshauri wa mumewe. Ni mnyonge na mwenye kutegemea mumewe katika mradi wake na ni chombo cha anasa cha kuburudisha mwanamume.

Mekacha anaendelea kutia msumari wa moto katika kidonda kwa kusema kuwa mwanamke ana 'mahitaji yasiyotimizika, ni mwenye wivu, mdhaifu na ndiye chanzo cha maovu yote katika jamii; hana mbeko, ni mwovu na shetani.' Mekacha hapa amechukua msimamo mkali na hasi katika kumsawiri mwanamke. Hatuelezei jinsi alivyofanya kufikia kauli hii kumhusu mwanamke na wala hakulinganisha utafiti wake na kazi nyingine ile au mtazamo mwingine. Ameegemea upande mmoja. Mekacha alijikita katika nyimbo ilhali utafiti huu umejikita katika ushairi ulioathiriwa na hisi za dini.

Momanyi (1998) ameutazama usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili Waislamu kama inavyobainika katika ushairi wa Kiswahili. Kazi ya msomi huyu imetupa mwangaza katika *Utendi wa Adamu na Hawaa,* huku tukilinganisha na *Paradise Lost.* Momanyi ameangazia jamii ya Waswahili



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

katika ushairi. Utafiti huu umetumia kazi yake kama akisi ya kazi hii kuangalia upya taswira ya mwanamke katika dini ya Kikristo pamoja na dini ya Kiislamu.

Ndungo (1998) ameangalia taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi za Kiafrika huku akijikita katika methali za Gikuyu na Kiswahili. Utafiti wake ni linganishi kama huu lakini alijikita katika methali. Utafiti wa Ndungo ulionyesha kuwa mwanamke ni mali ya mwanamume, ni kitu dhaifu, asiyeaminika, mdanganyifu na mwenye hila.

Knappert (1979:6) anaendeleza dhana hii hasi ya mwanamke:-

> ....Mungu aliumba mwanamume akitaka sana amwabudu.
> Mwanamke alimuumba ili atunge mimba na azae...
> Mwanamke anawakilisha matakwa ya kiulimwengu ya watu, tamaa ya ashiki na kufurahia watoto..

Knappet hapa alirejelea dini, lakini hakuilinganisha na nyingine wala hakujikita katika maandishi mahsusi ya fasihi ambayo utafiti huu umezingatia. Nukuu hili kwa hakika linampa mwanamume mamlaka makubwa, huku likimfanya mwanamke jaa na busati la kupangusia matope. Utafiti huu umetazama maoni haya ili kuona kama bado yana mashiko au yamepitwa na wakati. Hivyo umejikita katika msingi wa dini ya Kikristo na Kiislamu, jambo ambalo halijashughulikiwa na wataalamu kama ilivyotajwa awali.

Shaaban Robert katika Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili asema:

> 'Mume ni mume ingawa gume gume,ana sifa za mtume.
>
> Na mke ni mke ingawa kikwekwe ana sifa zake.'

Tunaona hapa kuwa mwanamume ametukuzwa ilhali mwanamke amedhalilishwa. Mtafiti alitazama upya mawazo kama haya, huku akimweleza mwanamke kwa tariki chanya.

Kimani (2003) alitafiti juu ya suala la dhuluma dhidi ya mwanamke katika fasihi ya Kiswahili. Alijadili aina mbalimbali za dhuluma zinazowakabili wanawake wa Kiafrika kama inavyojitokeza katika kazi teule za fasihi. Utafiti huu haukuwa linganifu na uliegemea upande mmoja. Ulionyesha picha hasi ya mwanamke. Mtazamo huu unabomoa, hauhimizi wala kutoa misingi ya kujaribu kumnasua mwanamke kutokana na ugandamizwaji katika asasi za ndoa, dini na utamaduni.

Okot P' Bitek, katika wimbo wa Lawino na Ocol, anasema

> .... Mwanamke wa Afrika, mfagiaji, anakandika,
>
> Sakafu na kuta kwa samadi na udongo mweusi.
>
> Mpishi, yaya, huku mtoto amefungwa mgongoni, anatapika.
>
> Mwosha vyombo, anapanda, anapalilia, anavuna.
>
> Mtunza vifaa, mjenzi, kijakazi, lori, mkokoteni, punda ...

Mwanamke wa Afrika, ni nini usicho kuwa?

Mawazo haya ya Okot yana mashiko siku hizi? Je, mwanamke wa Kiafrika bado amefungwa minyororo ya ugandamizwaji kama anavyosema P' Bitek? Mtafiti amemsawiri mwanamke upya ili kuona kama fikra hizi zimebadilika.

## 1.2 SUALA LA UTAFITI

Utafiti huu umeshughulikia taswira ya mwanamke katika *Paradise Lost* (Milton 1667) na *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* (Abdalla 1971). Kutokana na utafiti jaribio, mtafiti alikuwa ameona kuwa kulikuwa na haja ya kumwelewa mwanamke upya, haswa katika misingi ya sanaa ya ushairi ulioathiriwa na dini. Kumekuwa na suitofahamu katika dini za Uislamu na Ukristo. Pengine kutoelewana huku hakuhitaji kuwepo,kwani chimbuko la dini hizi ni moja, zote ni za uzao wa Ibrahimu.Dini hizi hazina uwiano wa mapokeo na hii ndiyo sababu ya utafiti huu, na ndiyo inayoruhusu udenguzi kufanya kazi. Utafiti mwingi uliofanywa juu ya mwanamke unaishia kumsawiri kama kiumbe anayedhulumiwa na dini, ndoa, na utamaduni.Aidha asasi hizi zinaishia kuonyesha mwanamke kama aliyedharauliwa , kupuuzwa na kuteswa. Tafiti hizi ni kama vile za Chacha (1998), Muindi (1990), Mule ( 1991), Ndungo (1998), Momanyi (1998) miongoni mwa nyingi.

Mtafiti ameona kuwa, kwa kiwango kikubwa, asasi hizi katika masuala ya kike zimetafitiwa kwa mtazamo hasi na hakuna utafiti hata mmoja uliotafitiwa kwa mtazamo chanya.Ni pengo hili linalomchapuzia mtafiti kuliziba.

Mtafiti amethibitisha hili kwa kuzingatia upya taswira ya mwanamke katika *Utendi wa Adamu na Hawaa* na *Paradise Lost*.

Kwa miaka mingi, picha anayosawiriwa mama wa kwanza wa binadamu ni ya mlaumiwa na mkosaji. Mtafiti amechunguza upya dhana hii kwa kurejelea tendi hizi mbili. Hali kadhalika amerejelea taswira za mwanamke katika Biblia na Korani kwa kumrejelea Hawaa.Vitabu hivi vitakatifu ndivyo vilivyokuwa msingi katika kuandikwa kwa tendi hizi hivyo urejeleaji wake katika utafiti huu ni muhimu. Aidha, amechunguza kama uwiano na usawiri wa mwanamke umejitokeza katika kazi hizi. Maswali yanayojibiwa na utafiti huu ni:-

(i) Je.asasi za dini , ndoa na utamaduni zinamdunisha mwanamke?

(ii) Je,mwanamke ni kiumbe duni na dhaifu?

(iii)Je,mwanamke anaweza kusawiriwa upya na kwa njia chanya ?

## 1.3 NADHARIA TETE

Mtafiti aliegemeza utafiti wake kwenye nadharia tete zifuatazo.

- Mwanamke anazo nguvu nyingi katika udhaifu wake.

- Kinyume na inavyochukuliwa na wengi, dini haimgandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi.
- Kuendelea ama kufaulu kwa maamuzi, mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke.

## 1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti uliongozwa na madhumuni yafuatayo :

a) Kubainisha ikiwa taswira zilizoko katika tungo hizi zinamwonyesha mwanamke kama kiumbe mwenye nguvu au dhaifu.

b) Kuonyesha jinsi taswira hizi zinavyoathiri mielekeo ya mwanamke.

c) Kuonyesha ikiwa usomaji mpya unaweza kumsawiri mwanamke upya.

## 1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Suala la mwanamke ni muhimu katika ulimwengu wa sasa. Hakuna njia ambavyo tunaweza kuepuka kuzungumzia juu ya mwanamke, kwani anachangia katika nyanja zote za maisha- kidini, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kadhalika. Mabadiliko mengi yametokea katika jamii ya ulimwengu na fursa mwanamke anayochukua.Ndiyo, kuna mzinduko mkubwa kuhusu nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya jamii. Hivyo basi kulikuwa na haja kuchunguza hali yake kwa kina zaidi.

Tafiti za awali hazijawa na ghera ya kulinganua tendi za kidini katika tamaduni tofauti za ulimwengu, haswa zilizoandikwa na waandishi wanaotofautiana kidini na kiisimu.

Kulikuwa na umuhimu mkubwa wa kuangazia jinsi asasi ya dini inavyochangia katika kumsawiri mwanamke. Aidha, mtafiti alikusudia kumshinikiza mwanamke awe mshiriki katika harakati hizi, bali si mtazamaji.

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa nguzo shakiki za kuegemewa/kutegemewa na waandishi ili waweze kuwaumba wahusika wao wa kike kwa mtazamo chanya. Kazi za waandishi hawa hatimaye zinaweza kuwa kichapuzi cha kubadilisha jamii, haswa zinazotawaliwa na itikadi za mfumo dume.

Taswira ya mwanamke kama chombo cha kumstarehesha na kumfurahisha mwanaume ni kizingiti kikubwa katika unisai hasa ikiwa wanawake wenyewe wanakubali na kuendeleza dhana hii. Mtafiti anawahimiza wanawake wasiufasiri tu ulimwengu, jambo muhimu likiwa ni kuubadilisha. Kama wasemavyo wanafilosofia kama Karl Marx , 'Watu wengi huishi wakijaribu kuufasiri ulimwengu, wachache sana hujaribu kuubadilisha.' Utafiti huu Unatarajiwa kuwafanya watu kutalii upya asasi na maono ambayo kwa muda mrefu huonekana kumgandamiza mwanamke.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu umeijikita katika usawiri upya wa mwanamke katika ushairi ulioathiriwa na dini. Mtafiti alichunguza tendi mbili, *Utendi wa Adamu na Hawaa* (1971) na *Paradise Lost* (1667).

Hizi ni kazi mbili tofauti kiwakati, kidini na kimazingira. *Utendi waAdamu na Hawaa* ni wa miaka ya 1970, misingi yake ni ya dini ya Kiislamu na mazingira yake ni ya Kiafrika.Hivyo basi Kazi hii twaweza kusema inajikita katika urasimi mpya. Mtafiti hakuchagua kazi zingine za Abdalatif kwani lengo lake lilikuwa kuchunguza tu maisha ya awali ya Adamu na Hawaa.Kuna tendi nyingi lakini hazimsawiri mwanamke wa kwanza.

Abdalla ameandika pia *Sauti ya Dhiki* (1973) na kuhariri Diwani ya Mohammed ya *Sikate Tamaa* (1980) na *Diwani ya Jinamizi* (1979) ya Zakwany

*Paradise Lost,* kwa upande wake, ni utendi ulioandikwa miaka ya 1600. Itikadi yake ni dini ya Kikristo na mazingara yake ni ya nchi ya Ulaya. Kazi hii inajikita katika urasimi mkongwe.

John Milton ameandika vitabu vingi kama vile:

- *On the morning of Christ's Nativity* (1629)
- *The reason of Church –Government*(1641)
- *Doctrine and Discipline of Divorce* (1643)
- *Of Education* (1644)
- *Paradise lost* (1667)

- *History of Britain* (1670)
- *Samson Agonists* (1671)
- *Paradise regained* (1671)

Mtafiti hakuchagua kazi nyingine za Milton, kwani lengo lilikuwa kumsawiri mwanamke wa kwanza kama sampuli kienzo ya wanawake wote wa baadaye. Utendi huu ndio uliotoa hili bayana.

Tofauti hizi ndizo zilizochangia kuchagua tendi hizi mbili. Zote zinarejelea suala la Adamu na Hawaa huko paradiso, kuanguka kwao na jinsi Ibilisi alivyowaghilibu.

Katika diwani hizi mbili, waandishi walishughulikia vipengele vya mwanamke kama mwenye busara na hekima, shujaa na mwenye uwezo mkubwa juu ya mwanamume.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

### 1.7.0 Utangulizi

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, nadharia ya ufeministi au unisai na nadharia ya udenguzi.Mtafiti alichunguza jinsi ambavyo mwanamke alisawiriwa *katika Utendi wa Adamu na Hawaa-na Paradise lost*. Hii ilimbidi atumie nadharia ya unisai. Hata hivyo, ili kumsawiri mwanamke kwa mtazamo mpya, mtafiti aliwajibika kuzitazama matini hizi na zingine alizorejelea kwa jicho la ndani, bila kurejelea muktadha.Hali hii ilihitaji nadharia ya udenguzi.

Kwa kuzioanisha nadharia hizi mbili, mtafiti amepata nadharia ya Unisai wa Kidenguzi. Hii ni nadharia changamano.

### 1.7.1 NADHARIA YA UDENGUZI

Katika fasihi, udenguzi una maana sawa na udhahania (Wamitila 2004:247). Udenguzi pia ni uumbuji. Wafula na Njogu (2007:110) wanaeleza kuwa mwasisi wa nadharia hii alikuwa Mfaransa Jacques Derrida (1967). Wanaeleza kuwa muwala au mshikamano wa kazi ya fasihi hujengwa kutokana na mchangamano wa tajriba ama uzoefu. Baadhi ya tajriba hizi zinapatikana katika kazi nyingine inayosomwa nje ya kazi hiyo.

Derrida aliamini kwamba neno lililopo huendele kuahirisha maana yake ya mwisho hivyo maana kukosa utangamano.

Njogu na Chimerah (1999: 13-14) wanafafanua kuwa sifa kubwa ya udenguzi ni uzingatifu wa lugha na matini. Udenguzi hupasua matini katika vipengele vyake vyote ili kuweka wazi kilichofichika.

Waitifaki wa udenguzi wana rai kuwa tunapohakiki matini, kinacholengwa hakiwezi kuhusishwa moja kwa moja na uhalisi au urejelezi. Msingi mkuu ni uwazaji au mawazo ya akili, bali siyo kitu kinachoweza kuguswa au kuonekana. Udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini kwa undani,

tunaweza kuielewa jamii na siyo lazima tuangalie muktadha wa matini ile. Lugha kama ishara ina uwezo wa kujifafanua. Udenguzi hushughulikia namna lugha na maana zinavyoingiliana na kufanya kazi pamoja.

**MIHIMILI YA NADHARIA HII**

1. Kazi ya fasihi haijifungi kwenye kaida za uhalisi, hasa za mandhari au jumuiya yake.
2. Matini ni chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha.
3. Sanaa inajitegemea na inapaswa kutathminiwa bila ya kuegemea vigezo vingine.

### 1.7.2NADHARIA YA UFEMINISTI

Wamitilia (2002) katika *Uhakiki wa Fasihi* anasema kuwa suala la haki na usawa wa wanawake lina historia ndefu. Kazi awali za suala hili ni kama katika kitabu cha nne cha andiko la Plato,. *The Republic* , kazi za Virginia Woolf- *A Room of Ones Own* (1984) na Mary Wollstonecraft- *Vindication of the Rights of Women* (1972) ambazo zilikuwa na mchango mkubwa katika kuanzisha harakati za ukombozi wa wanawake.

Kazi ya Simone de Beauvior ilikuwa na mchango mkubwa katika msingi wa

uhakiki wa kifeministi. Katika kitabu chake, *The Second Sex* (1972), Beauvior anashambulia na kukosoa baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Asasi hizi ni ndoa, dini na utamaduni.Beauvior anaishambulia mikabala ya kitamaduni inayomwangalia mwanamke kama kitu hasi, huku ikimchukulia mwanamume kama binadamu kielelezo bora.

Utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha mwanamke kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kuikubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa kijamii cha kuuendeleza utamaduni huo hasi.

Ndoa ni asasi mojawapo ya kiutamaduni inayoendeleza ugandamizaji wa wanawake. Asasi yenyewe imejengwa kwenye imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume na kuishi kumwangalia mwanamke kama chombo tu.

Beauvior anasisitisa kuwa asasi kama dini inatilia mkazo au nguvu itikadi ya kiume inayopatikana katika jamii nyingi. Asasi hii inaishia kuzipa nguvu mpya tamaduni dhalilishi dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya matamko ya kidini.

Mary Ellman, mhakiki wa kifeministi wa Kimarekani anaangazia jinsi wanawake walivyosawiriwa kwa namna mbalimbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwandishi alimulika pia jinsi baadhi ya waandishi wa kike walivyoendeleza usawiri huu hasi wa wanawake katika kazi zao. Hali hii inatokana na wao kukulia kwenye jamii inayotawaliwa na itikadi ya mfumo wa kuumeni na kuishia kufyonza baadhi ya mitazamo kumhusu mwanamke ambayo inakisiwa kwenye kazi zao.

Betty Friedan katika *The Femine Mystique* (1963) anachangia kuzuka kwa hisia za kifeministi Marekani. Friedan anayachunguza maisha ya wanawake ambayo kwa kiasi kikubwa ni mzingile, siyo tu kwa wanaume, bali pia kwa wanawake wenyewe.Mwandishi huyu anasema kuwa kutoyaelewa maisha hayo kumebakia msingi mkubwa wa hali ya maisha ya wanawake kwa jumla.

Kate Millet katika *Sexual Politics* (1977) anaishambulia vikali kazi ya waandishi maarufu wa kiume kutokana na jinsi wanavyowasawiri wahusika wao wa kike.

Kate anabainisha kwamba miundo ya kijamii pamoja na asasi zake vinashirikiana kumdunisha mwanamke.Mwandishi huyu pia anaishambulia mikabala ya Saikolojia Changanuzi inayohusishwa na Sigmund Freud – kwa kuwa na upendeleo mkubwa wa mfumo wa kuumeni. Freud alisema kuwa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

mtoto wa kike anaanza kujichukia mara tu anapotambua kuwa hana kiungo cha kiume. Hali hii husababisha kile alichokiita'wivu wa zubu.' Millet anadahili kuwa wivu uliopo ni wa uwezo alionao mwanamume kutokana na muundo wa kijamii. Mwanamke anakuwa na wivu wa kinachoashiriwa na hilo zubu, wala siyo zubu kama kiungo cha mwili (Wamitila: 2002).

Wahakiki wa kifeministi wanaendelea kukopa mawazo na mikabala kutoka shule nyingine za uhakiki kama vile Umarx, Saikolojia Changanuzi, Semiotiki, Udenguzi na Uhemenitiki. Mawazo haya yanatiliwa nguvu na Toril Moi kwenye kitabu chake cha *Sexual/ Textual Politics* (1985).

Moi katika kitabu hiki anayachunguza mawazo ya waandishi kadha wa kifeministi wa Kimarekani, Kiingereza na Kifaransa. Moi anaeleza kuwa mwana ufeministi wa Kifaransa Helen Cixous anaelekea kuonyesha kuathiriwa na Jacques Derrida na Jacques Lacan. Athari hizi zinajitokeza katika mawazo ya kiuwili kuelezea misingi ya itikadi ya kiume katika jamii. Mathalan;

| <u>Mwanamume</u> (ubabe) | <u>Mwanamke</u> (upole) |
|---|---|
| Jua | Mwezi |
| Baba | Mama |
| Kichwa | Hisia |

Hellen anaeleza kuwa kiini cha utaratibu huu ni tathmini za kiume zinazomwangalia mwanamke kama Wingine hasi.

Wamitila (2003:352) anaeleza Wingine kama dhana inayotumiwa kubagua kundi fulani la watu, mtu, au asasi.

## MIHIMILI YA NADHARIA YA UFEMINISTI

Wafula na Njogu(2007), Wamitila(2002)(2003) na Njogu na Chimerah(1999) wote wana maono sawa kuwa Ufeministi ni dhana inayojumuisha mikabala mbalimbali ya kiuhakiki ambayo, licha ya tofauti zake, inaelekea kukubaliana kwenye masuala kadha na malengo yake ya kimsingi.

Wafula na Njogu (2007:12) wanasema kuwa nadharia ya Ufeministi inaweza kubainishwa katika matapo mawili makuu. Matapo haya ni:

[i] Kimaeneo

[ii] Msisitizo na mielekeo maalumu na mahsusi

**Kimaeneo**

Katika tapo hili wanawake kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu wanasisitiza masuala mbalimbali yanayowakabili-sehemu hizi ni kama vile Marekani,Ufaransa ,Uingereza, na Afrika.

[a] Wafaransa

Wanawake wa Kifaransa wanatilia mkazo lugha ,utafiti wao unalenga katika kufafanua namna lugha inavyomtolea maana mtumiaji wake.Wanadai kwamba lugha inavyotumika ni zao la taasubi za kiume-inampendelea mwanamume zaidi kuliko mwanamke.Jazanda zenye kuelekeza uwezo,nguvu, na mamlaka ni za kiume na ilhali zenye kusawiri ulegevu na kutoweza ni za kike.

[b] Wamarekani

Wanakubaliana na Wafaransa kuhusu lugha.Wanaongezea kwamba wanawake wana namna yao na ya kipekee ya kuandika na kujieleza.Pia wanasema kwamba kuna dhamira zinazorudiwarudiwa katika tungo za wanawake. Wanashughulikia kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake kwa wanaume maalumu zinazoongea juu ya wanawake.

[c] Waingereza

Wanaona dhana yao kuwa ya kisiasa .Wanafikiria kwamba wenzao wa Kimarekani wanazungumzia zaidi masuala ya kihisia na kisanaa na kusahau historia na siasa .Kwao,mambo ya historia na siasa ndiyo huathiri maendeleo ya wanawake.

[d] Waafrika

Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake.Miongoni mwa vitengo vya utamaduni ni:

[i] Kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke na mzazi wa mwanajamii.

[ii] Tohara na ukeketaji wa wanawake

[iii] Kimya cha kulazimishwa.

[iv] Desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa.

### Mirengo ya Ufeministi wa Kiitikadi

Wakiwanukuu Adamson, Bouchier,Briskin na McPaul,Wamitila(2002, 2003), Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa mitazamo ya Ufemimisti wa Kiitikadi ni mitatu

[a] Ufeministi huru

Hutetea usawa kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote za maisha.Huitwa wakati mwingine Ufeministi wa kibepari. Mkondo huu hushikilia kwamba maadamu wanadamu wameumbwa kuwa viumbe sawa, wote, wake kwa wanaume, wanapaswa kuwa huru kuendeleza majukumu na malengo yao.

[b] Ufeministi wa Kiharakati

Huu huchukulia mwanamume kama adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Waitifaki wa mkondo huu wanaamini kuwa uwezo wa kuzaa wa mwanamke ndio ambao hutumiwa na mwanaume kumdhalilisha na kuutawala mwili wake. Kwa hivyo, ili wanawake waweze kujitawala katika nyanja zote za maisha wanahimizwa kushirikiana wao kwa wao hata kimapenzi.

[c] Ufeministi wa Kijamaa

Ufeministi wa Kijamaa hulenga kukosoa ujamaa wa kimapokeo ambao, licha ya kudai kwamba msingi wa unyonyaji ni jamii ya kiutabaka inayompa uwezo mwenye kumiliki njia kuu za kuzalisha mali ; kutumia mali hiyo kadiri ya uwezo wake , huendeleza utabaka na unyonyaji katika misingi ya kijinsia. Ufeministi wa kijamaa unawahimiza wanaume kushiriki katika malezi ya watoto na kadhia nyingine ambazo kimapokeo zimechukuliwa kuwa kazi za wanawake.

Aidha Wamitila (2003) anabainisha Ufeministi wa kibidhaa, Ufeministi wa kidhanaishi, Ufeministi wa kiutamaduni, na Ufeministi wa kiuyakinifu.

Mtafiti hakujibana na mtazamo mmoja wa kifeministi , kazi ililenga karibu mitazamo yote.

**Mihimili ifuatayo inalenga ufeministi kwa ujumla:**

(i) Fasihi ni jukwaa la kuelezea hali inayomkumba mwanamke ili aweze

kueleweka na wengi.

(ii) Kuwasawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na uana. Inapigania jamii mpya yenye misingi katika amali za kibinadamu.Baadhi ya amali ni za kike na za kijadi na ambazo zinadharauliwa katika jamii ya sasa.

(iii) Kuhamasisha utungaji wa kazi za sanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa, wanawake ambao hawawategemei wanaume ili wajitambulishe.

(iv) Kukuza na kuendeleza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

(v) Kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona,na uhusiano wao na watu wengine.

(vi) Kuvumbua na kuweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake na ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamume.

Manufaa muhimu ya nadharia hii kama asemavyo Wafula (2007: 95) ni kwamba inapigania usawa miongoni mwa wanadamu na inaonyesha udhaifu wa mfumo wa kuumeni. Inatetea uhuru wa mwanamke kwa kudai kuwa ana haki za kufurahia haki zote za kibinadamu.

### 1.7 .3 MIHIMILI CHANGAMANO: UNISAI WA KIDENGUZI

Baada ya kuoanisha nadharia ya Unisai na Udenguzi, mtafiti aliweza kupata mihimili changamano ifuatayo ambayo ilimwongoza katika utafiti huu:

(1) Maswala yanayomhusu mwanamke katika matini yanaweza kuelezeka bayana bila kurejelea muktadha.

(2) Matini ya Unisai wa Kidenguzi yanajitegemea na yanapaswa kutathminiwa bila ya kurejelea vigezo vingine.

(3) Unisai wa Kidenguzi ni uwazaji au mawazo ya akili,na siyo kitu kinachoweza kuguswa au kuonekana.

(4) Matini ya Unisai wa Kidenguzi haijifungi kwenye kaida za uhalisi wa mandhari au jumuiya yake.

### 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulijikita maktabani. Usomaji wa kina ulifanywa katika kazi zilizoteuliwa ili kubainisha jinsi mwanamke alivyosawiriwa. Ili kupata maelezo kuhusu waandishi, mtafiti alizingatia maandishi mbalimbali kwenye maktaba, upekuzi wa vitabu mbalimbali na majarida yaliyohusika moja kwa moja na utafiti huu yalisaidia katika kueleza usawiri wa mwanamke.

Vitabu vilivyokuwa na masuala ya ufeministi vilisomwa kwa undani, huku baadhi ya mawazo yaliyohusiana na mada yakinukuliwa. Kitabu Kitakatifu-

Biblia, kilitufaaa kwani masuala mengi yaliyohusu hadhi ya mwanamke yalipatikana mle.Ulinganishaji wa masuala husika na yale katika vitabu teule ulifanywa na kunakiliwa. Haya yalikuwa mufti katika usawiri upya wa mwanamke.

Ukusanyaji wa data ulihusu pia upekuzi wa vitabu mbalimbali na ukadiriaji wa nadharia ambazo zilifaa katika utafiti huu.

Data za kimsingi zinazohusisha kazi hii ziliteuliwa. Ushairi ulioteuliwa umechambuliwa pamoja na itikadi za watunzi.

### 1.8.1UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Data kutoka tendi husika zilizoteuliwa ,vitabu , makabrasha na majarida yaliyosomwa zilichambuliwa kulingana na masuala ya utafiti.Data zote zilizomsawiri mwanamke kwa njia chanya ziliwekwa pamoja na kuchanganuliwa chini ya mada anuwai. Zingine zilihitaji unukuzi ili kutoa ujumbe husika waziwazi .

Tendi husika ziliandikwa chini ya misingi ya Ukristo na Uislam-hivyo urejeleaji wa Biblia na Korani ulifanywa katika kuwasilisha data.Mashairi yaliyomsawiri mwanamke yaliyohusiana na mada yalinukuliwa, na mambo muhimu yaliyojitokeza katika mashairi haya yaliainishwa. Ulinganuzi wa taswira ya mwanamke katika tendi zote ulifanywa.

Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulifanywa kinathari.

## SURA YA PILI

## 2.0. HISTORIA YA JOHN MILTON

### 2.1.1 Utangulizi

Ili kuweza kuelewa bayana utendi wa *Paradise Lost* (1667), ambao umesifika kama utunzi wa upeo wa juu (Lois 1986), hatuna budi kwanza tumwangalie mtunzi, John Milton. Utendi huu ni kilele cha uandishi wake kwani alikuwa ameandika vitabu na makabarasha (pamphlets) lakini hakuna mojawapo inayosifika kama utendi huu(Bradfold 1992). *Paradise Lost* (1667) ni utendi uliochapishwa awali katika jumla ya vitabu kumi, lakini katika toleo la pili la (1674), ukachapishwa ukiwa na vitabu kumi na mbili.

Kazi yoyote ya fasihi haizuki katika ombwe tupu (Senkoro 1988), (Njogu na Chimera 1999), bali huwa ni mkururo wa tajriba za mwandishi pamoja na kadhia zilizomsibu. Hizi ni kama vile: Ukoo na aila yake, malezi, elimu, mazingira alimokulia, ndoa zake, matukio ya kijamii na kihistoria, mikondo ya siasa na utawala, itikadi zake na fauka ya yote, matamanio, falsafa na ndoto zake Katika maisha. Mtafiti aliabiri haya ili kuona jinsi yalivyomwathiri Milton katika kuandika utendi huu (juu ya mwanzo wa jamii ya wanadamu).

Mengi yameandikwa, mengi yanajulikana kuhusu msomi na mshairi huyu maarufu katika fasihi ya Uingereza na ulimwengu kwa jumla.Ili kuibua historia ya Milton, mtafiti alirejelea kazi za waandishi anuwai mathalan David

Loewestein (1993), Richard Bradford (1992) Lois Potter (1986), Sampson Low (1977) na Merritt Y. Hughes (1957) miongoni mwa kazi zingine.Historia hii ilioanishwa na utendi wa *Paradise Lost*.

Wakati Milton alipoandika utendi huu, alikuwa kipofu na umri wake ulikuwa miaka hamsini. Alikuwa amekerwa na ukengeushi wa kanisa na tawala za kifalme za wakati huo. Alijizatiti kuandika utendi huu wa kipekee unaoangazia ukweli wa Utukufu wa Mungu (Loewestein 1993). Hii ilikuwa ni baada ya kuanguka kwa utawala wa kidemokrasia huko Uingereza. Alijaribu kuunda paradiso ya aushi na kuthibitisha matakwa na njia za Mungu kwa wanadamu. Kazi na maisha yake kabla ya uandishi wa utendi huu yaweza kukadiriwa kama matayarisho na maono juu ya utendi huu ambao unazungumzia mada hii ya utakatifu- kuumbwa kwa binadamu wa kwanza, kuanguka na matokeo yake.

### 2.1.2 UKOO WAKE NA ELIMU

Milton alizaliwa tarehe 9/12/1608 katika mtaa wa Breadstreet Uingereza. Babake alikuwa mtu wa tabaka la kati na alikuwa mnukuzi, mthibitishaji rasmi, wakili na mkopeshaji pesa. Alikuwa na dada yake, Anne, aliyezaliwa 1601. Dada huyu aliolewa na Edward Philips. Mamake yao alikuwa Sara Jeffrey.

Wavyele wake walitoka katika madhehebu ya Protestanti na hivyo Milton alibatizwa katika kanisa la kiprotestanti huko Uingereza.

Milton alisoma katika shule ya Mtakatifu Paulo, huko London (1620-1625), na baadaye akajiunga na chuo cha mafunzo ya dini huko Cambridge miaka ya 1625 -1632. Aliona mitaala ya pale ikiwa ya kiwango cha chini. Alijitokeza katika midahalo na majadiliano ya hali ya juu yaliyohitaji upevu wa fikra na uwazaji wa kindani. Kwa mfano, alizua mjadala ikiwa elimu huwafanya watu wawe na furaha kuliko ujinga unavyofanya. Mijadala na mabishano kama haya, bila shaka, yalimtayarisha katika kuandika *Paradise Lost*, ambamo tunaona mbinu hizi zikijitokeza bayana. Alipata shahada yake ya B.A mwaka wa 1629 na baadaye mwaka wa 1632 akafuzu uzamili.

Baada ya mahafali ya Cambridge, aliendelea kusoma vitabu vilivyoandikwa na waandisha mashuhuri wa Kigiriki, Kilatini na Kiitaliano. Hii ilimpa fursa ya kuendeleza hekima yake na uelewaji wa maswala ya kihistoria, kisiasa na kidini.

Kwa muda wa miaka mitano, kutoka 1632-1638, alikaa na wazazi wake huko Horton, karibu na Windsor, katika nyumba iliyompa fursa mwafaka ya kusoma, kuandika na kuwaza. Baada ya kifo cha mamaye, Milton alipata ruhusa na udhamini wa baba yake kuzuru nchi nyingi za bara Ulaya. Ziara hizi kwa

msomi ziliweza kupanua akili, kumpatia hekima na tajriba mwafaka. Milton alitembelea nchi kama vile Ufaransa, Italia na Uswisi. Katika safari hizi, alikutana na Hugo Gratius,ambaye alikuwa mwandishi maarufu wa Kidachi, mwanasheria na mwanathiolojia na Galileo. Galileo wakati huu alikuwa kipofu na mfungwa. Milton amemtaja katika *Paradise Lost*.

Kote alikotembelea, Milton alipokelewa vizuri na walezi, maulama, na washairi katika akademia na vyuo anuwai. Hii ilizidisha imani yake kuhusu usawa na thamani ya mwanadamu, uhuru na haki ya kujieleza. Akiwa katika safari hizi, kulizuka mapigano huko Uingereza na akaghairi kuendelea kutembea. Aliona shida kuendelea kusafiri ilhali raia wenzake walikuwa wanaendelea kupigania usawa na haki nyumbani.

Aliporejea Uingereza, alijihusisha na ukufunzi wa kibinafsi ambapo alifunza mpwa wake, pamoja na wanafunzi wengine elimu ambayo aliona ilihitajika kwa washairi kama yeye- elimu kamili ya Sanaa na Sayansi. Kabrasha lake: *Of Education* (1644) linaonyesha ratiba ya mafunzo aliyodokezea- kwamba elimu ilipaswa kuleta mabadiliko na mtazamo mpya wa mtu katika maisha. Si ajabu basi *Paradise Lost* inapekua mahusiano ya ukufunzi. Tunaona katika kitabu cha 1:19 mshairi akimsihi Muse  amfunze:

....Nifunze,

Kwani wewe wanijua.

(Muse katika tamaduni za Kigiriki alikuwa ni Mungu wa kike kati ya watoto 9 wa Zeus walioulinda na kuendeleza ushairi, nyimbo, dansi na kadhalika). Hali ya kufundisha inapatikana pia katika kitabu cha 5-8 ambapo malaika Raphael anamfunza Adamu. Hali kadhalika, baada ya kuanguka kwa mwanadamu, tunaona malaika Mikaeli akimfunza Adamu majaribu ya historia.

Tangu akiwa mwanafunzi, Milton aliandika tendi za kimaadili na alijihisi kama mshairi –rasuli. Aliona kama Mungu amempa kipawa cha ushairi ili aweze kueneza mafundisho yake na kufafanua njia na matakwa ya Mungu kwa walimwengu.

### 2.1.3 MATUKIO YA KIHISTORIA NA KISIASA NA NAMNA YALIVYOMWATHIRI MTUNZI

Wakati Milton alipozaliwa, kuna matukio muhimu ya kihistoria na kisiasa yaliyokuwepo hadi yeye kuandika *Paradise Lost* mpaka alipokufa mwaka wa 1674. Matukio haya ni katika Uingereza na Ulaya kwa jumla. Milton alizaliwa Disemba 9, mwaka wa 1608 wakati wa utawala wa mfalme James wa

Kwanza, aliyetawala kutoka 1603- 1625. Ni wakati huo (1609-1611) ambapo mwandishi mwingine mashuhuri William Shakespeare, alikuwa anaandika vitabu vyake.

Katika mwaka wa 1610, mwanasayansi Galileo alitoa uvumbuzi wake – kuwa ni dunia inayozunguka jua na wala siyo jua linalozunguka dunia. Tunajua kuwa uvumbuzi huu ulimweka pabaya na kanisa Katolik,i kwani waliona kitendo hiki kama kufuru. Milton alipokuwa katika safari za bara Ulaya, aliwahi kukutana na mwanasayansi huyu (kama tulivyotaja hapo nyuma) akiwa kipofu na mfungwa. Milton amemtaja Galileo katika *Paradise Lost* na bila shaka uonevu huu wa kanisa, wa kutoruhusu uhuru wa kuwaza na kujieleza ulichangia pakubwa katika kuandika *Paradise Lost*.Katika utendi huu, tunaona akieleza kuwa hata Mungu alipowaumba binadamu wa kwanza, aliwapa uhuru wa kuamua na kuchagua, wala hakuwafanya makaragosi wake.

Mfalme James wa kwanza alifariki mwaka 1625 na ni wakati huo ambapo Milton alikuwa amejiunga na Christ's College.Ni wakati huo pia ambapo mfalme Charles wa Kwanza alishika hatamu za utawala, na kumwoa Henrietta Maria wa Ufaransa. Mfalme Charles wa Kwanza alitawala kutoka 1625-1649. Alivunja bunge mwaka wa 1629 na kuanza kutawala peke yake. Wakati huo Milton alikuwa anafuzu katika shahada ya B.A huko chuo cha Cambridge.Charles wa Kwanza alitawala bila bunge hadi 1640. Bila bunge ni

wazi kuwa demokrasia ilikuwa imezikwa katika kaburi la sahau. Kama tulivyotaja hapo awali, Milton alitetea uhuru wa kujieleza na uchaguzi na akahimiza uhuru wa dhamira / nia safi. Alishuku asasi na tawala zilizojitwalia mamlaka, akipendekeza mamlaka kutoka Biblia kama inavyobainika mwisho wa *Paradise Lost*. Mfalme Charles wa Kwanza anasimuliwa kama kabaila aliyefinya uongozi wa kiraia. Mwaka wa 1637, tunaona mtafaruku juu ya ndarahima za mauzo ya vitabu vya maombi ambayo alikuwa amewashurutisha Waskot (Scot) kununua. Ni mwaka huo huo ambapo pia mamake Milton alifariki.

Milton aliunga mkono maasi ya kiraia yaliyozuka na aliandika makabrasha na vitabu vingi vya dini, akikashifu nguvu za maaskofu na akihimiza mabadiliko ya kijamii, elimu bora na uhuru wa uandishi wa habari. Baada ya Charles Wa Kwanza I kuuliwa na jeshi la kiraia kwa kukatwa kichwa, Milton aliandika kabrasha- *The Tenure of Kings and Magistrate* (1649) akishangilia tukio hilo aliloliona la kizalendo na kishujaa.Alipuuzilia mbali wazo kuwa kulikuwa na koo bora au watu watakatifu kushinda wengine. Katika kabrasha hili, alisema kuwa raia walikuwa na haki ya kung'oa na ikibidi kumuua mtawala aliyetumia cheo na mamlaka yake vibaya. Kazi hii ilimpa hadhi kama mpigania haki za raia, na Cromwell alimpa kazi kama katibu wa juu wa Lugha za Kigeni katika baraza la mawaziri. Cromwell ndiye aliyekuwa ameshika hatamu baada ya Charles wa Kwanza. kazi ya Milton kama

mwandishi, mtetezi wa serikali ya mageuzi ilisaidia sana kuibua na kuendeleza kipawa chake cha uandishi na hili lilichangia katika uandishi wa *Paradise Lost.*

Cromwell alifariki mwaka1658 na mwaka mmoja baadaye utawala huu wote wa kiraia ulianguka, na utawala wa kifalme ukarudi. Wengi waliounga mkono utawala wa kidemokrasia wa Cromwell waliuliwa, na Milton aliponea chupuchupu. Wakati huo, akiwa kipofu, alijikuta katika mikondo mizito ya kisiasa na ilibidi ajifiche.

Alijikuta katika hali ya kutengwa, na ulimwengu wake ulikuwa wa giza. Athari za hali hii zinajitokeza katika *Paradise Lost* kama tutakavyoona baadaye.

Milton alipofuka kabisa mwaka wa 1652, lakini hili halikukatisha kipawa chake cha uandishi kwani hata katika hali hii aliandika vitabu na makabrasha mengi kama vile *Paradise Lost* (1667), *History of Britain* (1970), *Paradise Regained* na *Samson Agonistes* (1671), miongoni mwa vingine. Aliweza kuandika kazi hizi kupitia binti zake wawili, Deborah na Mary.

Baada ya kuporomoka kwa utawala wa kiraia ambao Milton alikuwa akiuona kama wa Mungu, na hivyo paradiso ulimwenguni, Milton alijikuta katika mazingira ya uhasama na vita na haya yalichangia katika uandishi wa utendi wa *Paradise Lost*. Katika utendi huu, tunamwona malaika Abdiel akiwa katika



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

mazingira kama haya ya uhasama miongoni mwa Shetani na malaika wake maaluni (kitabu cha 5).

Mazingira haya hata hivyo hayakubadili nia na falsafa yake kama mtetezi wa haki na ukweli na 'Mshari- Nabii'. Ukweli aliuona kama nguvu zisizoweza kuzuilika, kama mto uliofurika ambao katu hauwezi kuzuilika na tope za tamaduni na mapokezi ya kimila.

## 2.1.4 UPOFU WA MILTON

Katika kitabu cha 7 katika *Paradise Lost,* Milton anasema kuwa anaishi 'Katika giza lililojaa upweke na hatari.' Hapa anaangazia siyo tu hali yake ya kisiasa baada ya ustawishaji wa utawala wa kifalme, bali pia upofu wake. Upofu huu unaonekana kuwa hatari na kuwa umemtenga na ulimwengu.

KENYATTA UNIVERSITY

Shida za Milton za macho zilianza mwanzo wa 1644 na kufikia Februali 6, mwaka wa 1652, akapofuka kabisa. Kinyume na Sahili katika riwaya ya *Kufikirika* ya Shaban Robert aliyeomba upofu na akaishi akiufurahia, upofu huu, kwa Milton ulimletea machungu na hata akaanza kuhisi ni kama kitubio kutoka kwa Mungu kwa kushangilia kuuliwa kwa mfalme Charles wa Kwanza, kama mahasidi wake walivyodai. Ikumbukwe kuwa Milton alijiona kama 'Mshairi- Nabii' na kuwa hiki kilikuwa ni kipawa kutoka kwa Mungu ili aeneze ukweli na njia za Mungu kwa wanadamu.Hivyo basi baada ya kupofuka

alianza kujihisi kama yule mtumwa katika Biblia aliyepewa talanta moja na badala ya kuiwekezea, akaenda akaificha mchangani (Mathayo 25:14-30). Hata hivyo Upofu wa Milton haukuwa kizingiti, bali ulimpa nguvu na ukakamavu kama mshairi. Alisubiri na kumwomba Mungu ampe nguvu katika unyonge wake. Katika hali hii, alijiona kama 'Mshairi kipofu- Nabii' na wito wake ukawa 'nguvu zangu zakamilika katika unyonge wangu' huku akirejelea Wakorintho wa pili 12:9-10. Mawazo kama haya tutakuja kuyajadili baadaye tutakapotazama usawiri wa mwanamke kama aliye na nguvu katika unyonge wake.

Milton alianza kutafakari upofu wake kama hidaya kutoka kwa Mungu na ishara ya utakatifu. Alihisi nguvu mpya za ushairi zikitoka ndani, labda baada ya kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Angeweza kuona mengi na macho ya kiroho ambayo mtu asiye kipofu hangeweza kuona. Katika kitabu cha kwanza cha *Paradise Lost* (1: 22-23), Milton anaangazia hii hali yake ya upofu anaposema:-

> "............. kilicho ndani yangu ni giza.
> Niangazie....."

Anamsihi Roho Mtakatifu amwongoze anapoanza kuenenda katika safari yake ngumu. Safari hapa ikiwa na maana ya kuandika ilhali ni kipofu. Anaomba nguvu na macho ya kuweza 'kuona' anapoandika utendi huu.

Katika kitabu cha 3:40-55. Milton anasikitikia hali yake ya sasa ya upofu, anaposema:

Majira hurudi,
Lakini kwangu hakurudi
Usiku wala mchana
Siwezi tena kuona
Kipupwe au kiangazi
Kinachonizingira ....
Ni mawingu mazito ya giza
Yakinitenganisha...

Na furaha na njia za binadamu
Yakiniziba....
Nisiweze tena kuona
Maandiko ya Kitabu Kitakatifu
Yalioandikiwa binadamu wote
Yakiniziba....
Nisiweze kuona au kueleza
Uzuri wa uumbaji
Yameziba....
Njia moja ya kupata hekima.

Naomba mwangaza wa mbingu,

Uniangazie ndani moyoni mwangu

Ufungue hekima ya akili yangu,

Uondoe ukungu machoni mwangu,

Niweze kuona na kueleza

Yasiyoonekana na macho ya kawaida. (T.M)

Maombi haya ya Milton yanatufungulia hisia zake za ndani na kutuelezea jinsi upofu wake unavyowiana na utunzi wake kwa uwezo na nguvu za Mungu. Kama asemavyo Ruo Kimani katika Tuki (2003) 'Utunzi wowote ni kioo cha ndani cha fikra za mtunzi'.

## 2.1.5 MAISHA YA NDOA

Katika kuhitimisha historia ya Milton, hatuna budi kuchunguza maisha yake ya ndoa, kwani yana uwiano na wahusika katika *Paradise Lost*. Lois Potter (1971:102) asema kuwa wahusika wote katika utendi huu ni wa kweli ila wale ambao wametashihisiwa kama vile Dhambi, Kifo na Vurumai. Yaani Milton alikuwa anaandika kuhusu wahusika wa 'kweli'. Je, mahusiano na tajriba ya Milton na wanawake yalimwathiri katika kumsawiri Hawaa kama ruwaza ya wanamke wote wa baadaye?

Katika mwaka wa 1640, Milton alihama kutoka St. Brides Churchyard akaenda kuishi mtaa wa Alderfate (Sampson Low 1977:16-17). Hapa palikuwa mahali patulivu, pa kupendeza na palikuwa na bustani nzuri.

Alihamia hapa pia akiwa na babake ambaye kwa wakati huu alikuwa mzee. Mama yake, Sara Jeffrey, alikuwa ameaga dunia mwaka wa 1637 na dadake Anne aliyekuwa ameolewa na Edward Phillips alikuwa amefariki mwaka wa 1631 na kuacha wavulana wawili. Katika makao haya aliishi na wavulana hawa pamoja na wengine aliokuwa akiwafunza elimu aliyoona bora. Wavulana hawa walikuwa na umri wa kati ya miaka 12 na16 na walikuwa wanafunzi wa bweni (dahalia). Bila shaka, nyumba hii ya wanaume na ghulamu ilihitaji mwanamke.

Katika matembezi yake ya starehe na biashara huko Oxfordshire, Milton alikutana na Mary Powell, kidosho wa miaka 17. Walichumbiana kwa majuma manne na akamwoa na kurudi naye nyumbani. Nikahi yao hii haikudumu kwani baada ya miezi michache ilitumbukia nyongo na Mary akarudi kwao. Milton alimbembeleza na kumsihi sana, lakini Mary hakughairi. Wakati huo, Milton, msomi aliyebobea, alikuwa na miaka 33 na labda tofauti hizi zilichangia mfarakano huo. Aidha, misimamo tofauti ya kisiasa kati ya wavyele wa Mary na Milton ilitonesha kidonda. Ni wakati huo ambapo Milton aliandika kabrasha *The Doctrine and Discipline of Divorce* (1943), akiunga mkono talaka.

Miaka minne baadaye, Mary alimrudia Milton aliyemkubali tu shingo upande. Walijaliwa Watoto wanne, Anne aliyezaliwa mwaka wa1646, Mary mwaka wa1648, John mwaka wa1651 na Deborah mwaka wa1652. Mama mtu huyu alifariki mwaka wa 1652 na kumwacha Deborah akiwa na umri wa siku tatu . Milton alioa mara ya pili mwanadada aliyeitwa Katherine Woodstock mwaka wa 1656, akiwa na umri wa miaka 28. Katherine alizaa msichana mwaka wa 1657 lakini mama na mtoto wakafariki mwaka wa 1658.

Milton akiwa mzee wa miaka 55 na tena kipofu, hakutamauka katika mahaba, kwani mwaka wa 1663 alioa mara ya tatu. Aliyekuwa na bahati wakati huu ni Elizabeth Minshull, banati wa miaka 24. Elizabeth alikuwa mpole na mwenye mapenzi na miaka 10 waliyoishi pamoja ilikuwa ya amani na utulivu.

### 2.1.6 BABA NA BINTI ZAKE

Uhusiano kati ya Milton na binti zake unaonekana haukuwa shwari. Katika wosia wake (haukuwa umeandikwa) anasema anawaachia tu mali ambayo alirithi kutoka kwa mke wake Powell, kwani hawakuwa na shukrani wala huruma. Mali yake yote iliyosalia alimrithisha mke wake wa tatu. Labda, bila kujua, Milton alikuwa analipiza udhia aliopata kutoka kwa mama yao Mary na watu wa familia yao aliowachukia mno. Ushahidi tunaopata kutoka kwa

Edward Philip, mpwaye Milton ni kuwa Milton alikuwa mkali na alikuwa na mahitaji mengi, hivyo angefaa alaumiwe kwa kuzoroteka kwa uhusiano na binti zake(Bradfold 1992). Mama yao alipofariki walikuwa na umri mdogo. Anne alikuwa na umri wa miaka sita, Mary miaka minne, na Deborah malaika wa siku tatu. Hivyo banati hawa walikua bila mama na malezi waliyopata ni kutoka kwa baba aliyekuwa kipofu na aliyehitaji usaidizi zaidi yao. Uhusiano kama huu ulikuwa wa fadhaa wasichana hawa walipoendelea kukua.

Japo Milton alikuwa kipofu, aliendelea kiandika na kusoma vitabu vya lugha tofauti. Alipoandika *Paradise lost* , alisaidiwa na Mary na Deborah, kwani Anne alikuwa mlemavu na kigugumizi. Wasichana hawa walifanya kazi kupita kiasi wakimsomea baba yao vitabu vya Kilatini, Kifaransa, Kiitaliano, Kigiriki, na labda Kiebrani (Walikuwa wanasoma kikasuku). Fauka ya kusoma, walinakili tendi na kabrasha zake kiimla. Kadhia hizi zingetosha kumchosha mtu mzima seuze wasichana hawa. Milton hakukumbuka kuwa wasichana hawa aliowatumia kama vyombo vya kazi yake walikuwa binadamu na walipolalamika, alikasirika na kuwakaripia, huku akiwaita waovu. Kuolewa kwa Elizabeth Minshull kuliokoa jahazi, kwani alipokuja, alielewa pande zote mbili. Alifanya mipango wasichana hawa wapate utarazaki wa ufumaji na udarizi, na kuajiri watu wa kumsomea na kumwandikia Milton kazi zake-Taswira

ya mwanamke inayojitokeza hapa ni ya mpatanishi na mwelewa wa masuala katika ndoa.

### 2.1.7 Athari za ndoa katika uandishi wa *Paradise Lost*

Je, tajriba za Milton na wanawake ziliathiri usawiri wa Hawaa katika *Paradise Lost*? Tunaona Milton akimsihi na kumbembeleza Mary Powell asirudi kwao. Hata akiwa kwao, Milton alituma nyaraka na washenga akimsihi arudi, lakini haya yote yakawa mjango. Vivyo hivyo katika *Paradise Lost,* tunaona Adamu akimsihi Hawaa asitembee peke yake, lakini Hawaa anapuuza na kusema ana uhuru wa kutembea na anaweza kujilinda na maovu. Anaenda na kukutana na Ibilisi na matokea yake twayajua. Milton katika falsafa yake alipigania uhuru wa uamuzi na tunaona Adamu akimpa Hawaa uhuru huu, japo alihofia madhara yake.

Baada ya kutengana na Milton miezi michache baada ya kuoana, ni Mary aliyechukua hatua miaka minne baadaye ili kurudiana na Milton, na alifanikiwa. Vivyo hivyo, baada ya maanguko ya Adamu na Hawaa na kufukuzwa kutoka Paradiso, ni Hawaa anayechukua hatua kurudiana na Adamu na alifanikiwa. Kurudiana kwa Milton na Mary hakukuwa kwa vigelegele, kama ambavyo kurudiana kwa Adamu na Hawaa kulivyokuwa – kwa machungu.

Tumehitimisha safari yetu ndefu ya kuibua mapisi ya John Milton. Tumetalii maisha yake tangu kuzaliwa, elimu na falsafa yake maishani, ndoa zake, matukio ya kihistoria na kisiasa na mchango wake. Japo alipofuka, hili halikuwa kizingiti katika uandishi wake bali kikanyagio cha kubobea zaidi. Kama alivyosema katika kabrasha moja: -

> 'kuwa kipofu siyo simanzi,
>
> simanzi ni kutoweza kuvumilia upofu.'

Aliandika tendi na makabrasha mengi kutetea demokrasia, uhuru wa vyombo vya habari na alionelea watu wangetenda wajibu wa Mungu, kungepatikana paradiso ulimwenguni. Mshairi na msomi huyu maarufu baada ya Shakespeare, alikufa kwa jongo tarehe 8 Novemba 1674 na akazikwa katika kanisa la Mtakatifu Giles, Crippiegate.

## 2.2.0 HISTORIA YA ABDILATIF ABDALLA

### 2.2.1 Utangulizi

Hakuna mengi yaliyoandikwa kuhusu maisha ya mwandishi huyu. Ni mshairi anayetambulika, haswa kwa kitabu chake *Sauti ya Dhiki* kilichochapishwa mwaka wa 1973.

Ameandika pia *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* (1971), ambacho ndicho mtafiti alikishughulikia katika tasnifu hii. Utendi huu ulohaririwa na Abdalahi Nassir ni hadithi inayokubalika na isiyopingika kuhusu mwanzo wa jamii ya ulimwengu. Zaidi ya kazi hizi mbili, Abdilatif amehariri Diwani ya *Sikate Tamaa* (1980) ya Said Ahmed Mohammed na *Diwani ya Jinamizi* (1979) ya Ali Salim Zakwany.

Amechapisha mashairi kadha katika magazeti ya Tanzania kama vile 'Napiga hodi'. Katika *Kioo cha Lugha* (1972) 'Nijile Taka Idhini' katika Ngurumo 12/4/1973, na 'Nishakaribiya' katika Ngurumo 25/8/1973.

Abdilatif aliwahi kupata tuzo la Jomo Kenyatta Foundation (Price for Literature) na pia tuzo la Diploma in Poesy na hivyo akapata cheo cha Ustadh (mwalimu wa mashairi).

## 2.2.2 MAISHA YA ABDILATIF ABDALLA

Je, huyu Abdilatif ni nani? Chacha (1980: 280) anatueleza kuwa Abdilatif alizaliwa tarehe nne mwezi wa Aprili mwaka wa 1946 katika mtaa wa Kuze,

huko Mombasa. Alilelewa na babu yake Ahmed Basheikh Bin Hussein tangu akiwa na umri wa miaka miwili. Huu ulikuwa ni ukoo wa ushairi na ni babu huyu pamoja na Ahmed Nassir (Juma Bhalo) nduguye, waliomsukuma Abdilatif katika bahari ya ushairi.

Ahmed Basheikh alikuwa mwalimu na mshairi. Alitunga na kuimba mashairi yake katika stesheni ya redio huko Mombasa. Kama ilivyo kaida ya watoto Waislamu, Abdilatif alipelekwa chuoni kusomea Korani. Baadaye aliendelea na mafunzo haya akiwa nyumbani.

Katika mwaka wa 1953 alianza masomo ya Utaratibu wa Kigeni katika shule ya Faza. Mwaka wa 1957 alimaliza sehemu ya kwanza ya shule za msingi na mwaka huo huo akahamia shule ya msingi ya Takangu pamoja na babu yake Ahmad. Mwaka wa 1962 alifanya mtihani wa KAPE, lakini hakufuzu.

Kuishi na babuye kulimpa tajriba za kutunga mashairi ambazo bila shaka zinajitokeza katika *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* na zaidi katika *Sauti ya Dhiki*. Babu yake alimpa fursa ya kuhariri mashairi yake kabla hajaenda kuyaimba katika idhaa ya redio huko Mvita. Aidha mashairi yaliyokuwa yanachapishwa katika gazeti la *Sauti ya Pwani* yalimpa mshawasha na mwamko katika utungaji wa mashairi.

Baada ya kumaliza darasa la nane, alipata ukufunzi wa kibinafsi akiwa nyumbani kutoka kwa mwalimu wa British Tutorial College. Baadaye alijiunga

na chuo cha utabibu katika hospitali kuu ya Mombasa. Hakuhitimu mafunzo haya kwani baada ya miaka mitatu baada ya kujiunga nacho, aliongoza mgomo akiwa na wakufunzi wengine, mgomo ambao haukuwa halali. Walidai kuwa chuoni hakukuwa na vifaa mufti vya kujifunza utabibu na kuwa maisha humo yalikuwa mabaya. Kukuru kakara hizi zilimpa fursa ya kuajiriwa kama Mhasibu Msaidizi katika Baraza laJiji la Mombasa.

Abdilatif alikuwa na msimamo thabiti kuhusu suala la haki za binadamu. Alichukizwa na ukandamizaji na dhuluma zilizoendelezwa na tawala za wakati huo. Alisoma vitabu vilivvyohusu wapiganiaji uhuru na kujinasibisha nao. Aliathiriwa na falsafa za Kimarx za ujamaa na maulama kama vile Fanon na Lenin, miongoni mwa wengi waliojishughulisha na uandishi wa masuala ya kisiasa. Kakake, Abdilahi Nassir, alikuwa na mshawasha mkubwa kwake katika mambo ya kisiasa.

Akiwa bado mfanyikazi wa Baraza la Jiji la Mombasa, Abdilatif alijiunga na chama cha K.P.U. Alikuwa mwanasiasa shupavu na aliandika makala ya chinichini kueleza siasa za K.P.U. Akiwa na wenzake, waliandika kisirisiri Kuhusu udhaifu wa serikali ya KANU na kueleza ambavyo ilikuwa imeshindwa kutekeleza ahadi ilizokuwa imetoa kwa wananchi wakati wa harakati za kupigania uhuru.

Mwaka wa 1968 aliandika makala 'Kenya: Twendapi', baada ya kukataliwa kugombea viti katika Baraza la Jiji la Mombasa. Kutokana na makala haya, alishikwa na kutupwa gerezani.

Alifungwa miaka mitatu kwa shutuma ya kuchochea raia wa Kenya kushika silaha kupindua serikali halali ya wananchi. Alitumikia kitubio hiki katika gereza la Kamiti na baadaye gereza la Shimo la Tewa. Aliandika *Sauti ya Dhiki* wakati huo.

Abdilatif aliachiliwa kutoka gerezani Machi 1972 na Agosti mwaka huo akaajiriwa kazi katika Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam. Alianza kazi kama Msaidizi wa Utafiti, akawa Mwana Utafiti Mdogo, Mwana Utafiti na hatimaye Mwana Utafiti Mwandamizi katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Aliendа Uingereza kwa masomo ya juu na akaajiriwa kazi huko.

Abdilatif alisalitiwa na rafiki yake aliyetoa ushahidi muhimu katika kesi yake. Vivyo hivyo, tunaona Adamu akisalitiwa na Hawaa na kuvunja sheria za Mungu katika *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa.*

## 2.3 Uwiano na utofauti wa waandishi hawa

Ni wazi kuwa John Milton na Abdilatif Abdala wana mengi yanayofanana na kutofautiana. Abdilatif ni Mwafrika Mkenya ambaye ni Muislamu na lugha yake kuu ni Kiswahili. Aliandika utendi wake katika karne ya 20 na ametumia Korani kama msingi wa mawaidha yake kuhusu habari za kuumbwa kwa

binadamu.Alijitolea kushutumu utawala uliogandamiza wananchi na alipata idhilali na hata kufungwa kwa kuelimisha wananchi juu ya haki zao. Ni msomi mtajika. Utendi wa maisha ya Adamu na Hawaa una beti 637 na umegawanyika katika sura au faslu sita.

John Milton ni Mwingereza na aliishi katika karne ya 16. Aliandika *Paradise Lost,* Hadithi inayosimulia chanzo cha binadamu na kuanguka kwao akirejelea Biblia. Alikuwa mpevu wa fikra na alishutumu tawala za kifalme na Uaskofu uliokosa uadilifu. Alipigania haki za binadamu na uhuru wa uandishi. Aliteseka kwa maoni yake na nusura auawe kama mhaini. Ni msomi na mwandishi mtajika katika fasihi. *Paradise Lost* ni utendi mkubwa unaojumlisha vitabu 12 na mishororo mingi sana. Lugha kuu ya Milton ni Kiingereza na utenzi huu umeandikwa kwa Kiingereza, japo umetafsiriwa katika lugha zingine kama vile Kilatini.

Mtafiti alitazama kazi za waandishi hawa katika tenzi zao zilizotajwa na kuaua jinsi walivyomsawiri Hawaa, kama dhana ghadi ya wanawake wote wa baadaye.

Mtafiti alitumia nadharia ya Unisai na Udenguzi, kwa pamoja akaziita Unisai wa Kidenguzi .

Ufeministi ulifaa kwani maswala husika ni ya kike. Hata hivyo yalihitaji kudenguliwa ili kupata ujumbe uliokusudiwa hivyo nadharia ya udenguzi.

# SURA YA TATU

## 3.0. UCHANGANUZI WA UTENDI WA MIASHA YA ADAMU NA HAWAA NA PARADISE LOST - MISINGI YA UNISAI WA KIDENGUZI

### 3.0.1 Utangulizi

Katika kuchanganua tendi hizi mbili, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Ufeministi na nadharia ya Udenguzi ambazo kwa pamoja ameziita Ufeministi wa Kidenguzi. Mtafiti aliangalia maswala yanayomhusu mwanamke katika matini hizi na Kuyaeleza upya kwa kuyadengua,hakujikita tu katika tendi hizi mbili ,bali pia katika Biblia na vitabu vingine alivyosoma . Hivyo kazi hii inaegemea mihimili ya Ufeministi inayochukua fasihi kama jukwaa la kuelezea hali inayomkumba mwanamke ili aweze kueleweka na wengi.

Hawaa ni ruwaza ya wanawake wote duniani, hivyo hali iliyomkumba ndiyo inayowakumba wanawake wote ulimwenguni.

Mtafiti alichunguza maswala yanayomhusu mwanamke na maana fiche katika matini hizi, kwani matini ni chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha(Tazama mihimili ya nadharia ya Ufeministi).

Kuna mengi yalioandikwa kuhusu paradise *lost,* hivyo mtafiti amechanganua utendi huu kwa kina zaidi. Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa umeshungulikiwa zaidi na maulama kama Chacha N. Chacha.

## 3.1. UCHANGANUZI WA UTENDI WA MAISHA YA ADAMU NA HAWAA

Utendi huu uliandikwa na Abdilatif Abdalla na kupigwa chapa na Oxford Univerty Press (1971). Ulihaririwa na Abdilahi Nassir.

Utendi huu umengawanyika katika faslu au milango sita na mwanzo wake una utangulizi na dibaji. Fauka ya haya , mwisho kuna sherehe au maelezo ya maneno mageni/magumu. Una beti 637. Abdilatif Abdalla ni Muislamu na ametumia Korani takatifu kueleza maisha ya wavyele wetu wa mwanzo, ambao ni Adamu na Hawaa. Huu ni utendi wa hali ya juu, kwani amechukua maandiko matakatifu na kuyaeleza kishairi bila kupotosha ujumbe wa Mungu.

Katika utangulizi, mhariri Abdilahi Nassir anaeleza machache kuhusu mtunzi. Asema kuwa utendi huu uliandikwa na Abdilatif Abdalla na nduguye, Ahmad Nassir Juma Bhalo . Umehifadhiwa kwa hati yake mwenyewe Abdilatif, katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam.

Abdilahi Nassir aeleza kuwa Abdilatif alizaliwa 1946 na, kwa kuwa alikuwa mtoto wa Kimvita, lugha aliyoitumia kuandika utendi huu ni Kimvita. Azidi kueleza kuwa alijaribu kutafsiri baadhi ya maneno ya Kimvita, mengi akayaacha vile vile, lakini akayapa maelezo katika sherehe.

Katika dibaji, mtunzi anasema kuwa anayotunga yanatokana na mafunzo aliyopewa akiwa chuoni. Kusudi kubwa la kutunga ilikuwa kueleza mwanzo wa wanadamu kwa kusimulia kisa cha Adamu na Hawaa. Ingawa ametumia



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

lugha ya Kiswahili kuandika utendi huu, mtunzi anaomba radhi kwa makosa yoyote yaliyojiri katika kitabu.

**Faslu ya kwanza**

Katika **faslu ya kwanza,** mtunzi atanguliza kwa kurejelea Mungu mwenye rehema, na asiye na mwanzo wala mwisho. Mungu huyu anamsifu kuwa hana mke, kaka wala dada, hana mfano na aliviumba vyote vilivyo duniani na mbinguni.

Katika ubeti wa 17, tunaona Mungu akiwaambia Malaika mipango ya usoni kwamba atamuumba binadamu. Binadamu huyu atamuumba kutoka udongoni na atatawala vyote duniani kwa niaba yake Jalali. Kinyume na malaika walioumbwa kwa nari na hukaa mbinguni, binadamu ataumbwa toka udongoni na atakaa aridhini.

Malaika walitoa hofu yao kuwa binadamu ataleta maasi na maangamio (ubeti wa 28)

Ataanzisha matata
Moto mkuu wa vita
Kwa husumu na kuleta
Damu kujimwaikia.

Katika ubeti wa 34, Malaika wanahofia kuwa binadamu ataharibu na kuichafua dunia.

Faslu hii inamalizika huku Mungu akiwajibu malaika wake kuwa anajua wasiyoyajua.

**Falsu ya pili**

Ni kuumbwa kwa binadamu kunakotokana na uwezo na nguvu za Mungu. Binadamu aliumbwa kimakusudi, kila kiungo chake kikiwa na wadhifa wake. Katika mwili wake, hakuna kiungo muhimu kuliko kingine, vyote viko kufu. Baada ya kukamilika kuumbwa, Mungu aliwaita malaika na wote wakamsujudia, ila Ibilisi. Ibilisi akiwa amefurikwa na kiburi na uovu, aliona hawezi kumsujudu kiumbe aliyeumbwa kwa udongo ilhali yeye aliumbwa kwa nari. Cha mno ni kwamba, Adamu yuaishi duniani na yeye Ibilisi mbinguni. Katika ubeti wa 59 asema:-

Yapasa vya aridhini
Kutii vilo mbinguni
Si vya mbinguni kuja chini
Adamu kusujidiya

Viumbe vingi, vya kike na kiume havimwasi Mungu, bali hutii amri zake. Ni shetani tu ambaye aliasi. Mungu alimwita Ibilisi na kumwambia kuwa mmoja wa watumwa wake angemkosea na Ibilisi akatoa laana kwa yule atakayeasi. Ibilisi hakung'amua fumbo la Mungu, hivyo alijilaani yeye mwenyewe.

Anahojiwa sababu za kukataa kumsujudu Adamu naye asema hangefanya hivyo kwani Adamu ni kiumbe dhaifu wakilinganishwa. Kutoka hapo Ibilisi alifukuzwa kutoka peponi, huku amekwisha hukumiwa.

Akiwa amejawa maringo na majivuno, Ibilisi anaomba apewe fursa ya kuwaghilibu insi. Ombi lake lakubaliwa na wote watakaokubali uongo wake wangeangamizwa katika ziwa la moto pamoja naye. Wale watakaokataa uwongo wa Ibilisi watawekwa peponi. Kutoka hapo alifukuzwa toka peponi hadi duniani, akatangetange apate watu wa kurubuni.

Mtafiti hakujikita katika nadharia moja ya Ufeministi, mihimili ilinguza nadharia zote.Ufeministi wa Kiharakati unaowahimiza wanawake kushirikiana wao kwa wao kimapenzi unapigwa vita hapa, kwani kila kiungo cha mwili kina wadhifa Wake - Mtafiti hakubaliani na ndoa za jinsia moja - Hili laungwa mkono na matini hii iliyoandikwa chini ya misingi ya dini.

**Falsu ya tatu**

Inaeleza kuwa baada ya Adamu kuumbwa, alipewa elimu na maarifa. Anatoa majina ya kila kitu kilichoumbwa. Alitoa majina kwa viumbe wa mbinguni na ardhini, majina ya nafaka, nyota, thurea na hata majina ya malaika, sifa zao, na kazi zao kwa Mungu wao.

Elimu na hekima hii ya Adamu iliwashangaza malaika waliofahamu sasa sababu za kusujudiwa kwa Adamu. Waliomba Mungu msamaha kwa kubishana naye. Aliwajibu kuwa alijua kile ambacho malaika hawakujua. Katika faslu hii, kutoka ubeti wa 128 mpaka 154 tunaelezwa kuwekwa kwa Adamu peponi. Tunafafanuliwa mandhari ya peponi na matunda anuwai yaliyokuwa mle:-Bustani nzuri, aridhi nzuri, mito iliyonukia manukato na kadhalika. Japo alipewa vingi na vizuri, alitamani mtu kama yeye wa kuongea naye. Alitaka aondokewe na upweke. Alilala na alipoamka, alimwona mwanamke mrembo, akamwita Hawaa na kumshukuru Mungu kwa kumuumbia alichotamani moyoni sasa. Katika ubeti 145, Mungu amwambia Adamu:-

> Nimeshakupa mwenzio
> Kaa naye ni mkeo
> Raha zote na pumbao
> Pepo kusistareheya

Ingawa Adamu ndiye mtangulizi wa kutoa majina:-Anatoa majina kwa malaika , vyote vilivyoumbwa akiwemo Hawaa,fursa hii anakuja kuipoteza pindi Hawaa anapomchezea akili. Kuzaa na kuwapa watoto majina kunampa Hawaa nafasi ya juu zaidi ya Adamu.

Wapenzi hawa wawili wanapewa mamlaka na nguvu juu ya vyote vilivyoumbwa, wanaambiwa waweza kula matunda yote, ila yale ya mti wa

katikati. Sababu kuu ya kukatazwa kula matunda ya mti ule ilikuwa kuona kama wanaweza kutii amri. Walisema wamesikia na watatii. Maisha yao peponi yalikuwa mazuri, matamu na ya raha mstarehe.

Adamu na Hawaa waliendelea kuishi peponi na wakati mmoja Hawaa akakawia kurudi kiamboni. Hili lilimtia Adamu kiwewe na Hawaa aliporejea alimsaili kuhusu hili. Hawaa alijitetea kuwa alikuwa mumo peponi, alimueleza Adamu kuwa aliona miti mingi yenye matunda matamu, miti ya tembo yenye maziwa mengi yanayozima kiu. Majumba ya kuajabia, vitanda vyeupe vya dhahabu na mengine mazuri.

Ajabu ni kwamba hakuona mti ulioharamishwa na Mungu. Mti ule, alisema Adamu una matunda ambayo Hawaa angeyala angebadilika na kuwa msichana mrembo. Hapa Adamu aliutia msumari wa moto kwenye kidonda kwani Hawaa hakutaka kuuona wala kuusikia. Wivu ulimyonga. Ubeti wa 182.

Nifanyeni mwanamke
Kwako wivu nisiweke
Sipendi mwenza wa kike
Kanami kuwa sawiya.

Hawaa alipendekeza wasitengane tena. Mti ule, uzaao wasichana unambughudhi sana Hawaa na habari zake hakutaka kutajiwa tena.

Katika pilkapilka zake, Hawaa alipata umbea kuwa mti ulioharamishwa na Mungu ni mzuri kuliko miti yote iliyobakia. Ni mti wa utambuzi, una vizazi na

Hawaa alijiuliza kwa nini Mungu hakuwaweka huko mbinguni kama malaika. Ukosefu wa madhila duniani, kama vile njaa na huzuni ndivyo vinavyomtinga Hawaa. Adamu alishangaa maoni haya Hawaa kayapata wapi kwani hakuna aliyeingia mle duniani. Ni bayana kuwa karubuniwa na Shetani. Mti ule kulingana na Hawaa, ungewafunza mema na mabaya.

Kulingana na Hawaa, wangalipaswa kuendelea kimaisha wasibakie pale udongoni.

Anaonelea ni bora wazae watoto wazidishe furaha yao. Watoto watapatikana tu kupitia kula matunda ya mti wa katikati.Adamu alishangaa vipi Hawaa aliweza kupata habari ile ila kupita kwa Shetani, anayemhadaa ili wavunje amri za Mwenyezi Mungu. Huku kutamani makuu si sifa ya kiungu.

Faslu hii inazidi kutueleza mazungumzo kati ya Hawaa na Ibilisi - Ibilisi anamshaswishi Hawaa atumie mbinu zote ili Adamu ale matunda ya ujuzi wa wema na uwi.

Anamwambia Hawaa kuwa Adamu ana njama za kuoa mke mwingine ndipo anakataa hoja ya kula matunda ya mti wa kati. Ubeti wa 295 unasema,

Vumili mwako moyoni
Uje uone machoni
Adamu huku peponi
Hurulaini kuowa.

Wazo la mitara linamtia Hawaa kiwewe na anamwomba Ibilisi amfunze tariki atakayotumia ili ampate Adamu kufanya analoliona muhali. Katika ubeti wa 304, Ibilisi anamshauri Hawaa:-

Tumia yako madaha

Maneno ya ufasaha

Iwe kwako ni silaha

Ya kike kuitumiya.

Kama tutakavyojadili baadaye, ubeti huu unaonyesha nguvu za kike ambazo wengine wataziita unyonge- labda hila , lakini hizi ni 'nguvu katika unyonge'.Nadharia yetu ya Unisai wa Kidenguzi inatuongoza kuona kwamba mwanamke anazo nguvu nyingi katika unyonge wake .Unyonge wake umesheheni hila –nguvu fiche. Madaha na maneno ya ufasaha si ulaghai, bali ni nguvu alizonazo mwanamke.Mhimili wa nadharia ya mtafiti kuwa fasihi ni jukwaa la kuelezea hali inayomkumba mwanamke inabainika bayana hapa.

Katika ubeti wa 305 mpaka 307, Shetani (Ibilisi) anazidi kutufunulia nguvu zingine za kike:-

Ubeti wa 305

Enenda kanene naye

Ya upole umwambiye

Tena kilio uliye

Hayo kikukataliya.

<u>Ubeti wa 306</u>

Kwake ulie kipenzi

Tone moja la majonzi

Litamtia majonzi

Na kukusikitiya

<u>Ubeti wa 307</u>

Kuiba wa mtu moyo

Si kwa nia nyingineyo

Cha mwanamke kilio

Chatia mtu ridhaa

Kama tulivyotaja awali, Mwanamke anapotaka jambo, hutumia ule 'unyonge wa kike', *maneno matamu ya kuongoa na kilio kama silaha.* Huu si unyonge bali ni hila na nguvu alizo nazo mwanamke, na asasi yake ni Hawaa, mama wa wanawake wote duniani. Taswira ya mwanamke inayojitokeza hapa ni ya kiumbe mwenye nguvu na hili linasadifu malengo ya utafiti ,aidha nadharia tete kuwa mwanamke anazo nguvu katika unyonge wake inasadifu.Kwa kudengua matini hii,ni wazi kuwa dini hapa imempa mwanamke nguvu za kisiri na kumwinua, katu haimgadamizi. Hii inapiga ndipo katika madhumuni ya utafiti.Kupata unachokitaka pasi kutumia nguvu ni mojawapo ya mbinu za kisaikolojia za kusuluhisha matatizo katika maisha.

## Faslu ya nne

Tunaona Hawaa sasa akitumia mbinu alizofunzwa na Ibilisi kumshawishi Adamu. Bila kujua, Adamu yuachukuliwa kitikiti mpaka chini ya mti wa kati na kwa ujasiri mwingi, Hawaa anafanikiwa kumlisha tunda lile la mti wa kati. Baada ya kuchutama na kula matunda, mara walijihisi wako uchi. Hatuelewi kwa nini wachutame wale matunda ilhali wangeyala wakiwa wima. Huku kuchutama kunaashiria kitendo zaidi ya 'kula' tunda, labda wakijua, au kufanya jambo lingine. Mbona wakajiona uchi, mbona wakawa na tahayuri? Hapa mtunzi Abdalatif katuachia tujijazie wenyewe:

Ubeti wa 368

Pamoja wakachutama
Baba na mwenziwe mama
Penye mti wa harama
Matunda wakajiliya.

Ubeti wa 312

Kwa haya na tahayuri
Watoke kwenye shajari
Tupu wakijisitiri
Majani kujizibiya.

Baada ya kutenda dhambi hii, dhambi hii ya mwanzo, Adamu na Hawaa walifukuziwa duniani na mwenyezi Mungu.

**Faslu ya tano**

Adamu na Hawaa wanajikuta duniani, dunia kavu isiyo na kitu na wanalaumiana kwa hali yao ya sasa. Adamu anamlaumu Hawaa kuwa ndiye aliyemshurutisha, kwa kilio chake, kula yale matunda haramu. Alifanya vile ili amridhishe Hawaa. Swali ambalo twapasa kujiuliza hapa ni hili, Adamu alikula tunda amfurahishe na kumridhisha Hawaa mkewe, je Hawaa alikula tunda kwa nini? Hakutaka kumridhisha wala kumfurahisha yeyote,bali alitaka kujua, alikuwa na moyo wa kutamani kugundua, alikuwa amechoka na hali yake na alitamani hali nyingine kushinda ile aliyokuwa nayo. Nadharia ya Unisai wa Kidenguzi inapiga ndipo, kwani matamshi haya yanaidhinisha kuwa mwanamke ni bora kumshinda mwanamume, na dini inampa hadhi kinyume na vile inavyofikiriwa na wengi. Hapa mwanamume anasawiriwa kama mjinga na anayetawaliwa na hisia zake – alionelea ni mufti kumkosea na kutomtii Mungu lakini amridhishe Hawaa. Mwanamke anasawiriwa hapa kama kiumbe mkakamavu na mwenye busara, kwani alililia tunda si amridhishe yeyote,bali atambue , ajue na aishi milele. Dini hapa basi inamwinua na kumpa hadhi. Hili linasadifu madhumuni na nadharia tete za mtafiti. Sura hii inaishia wavyele wetu hawa wa kwanza wakiomba toba kwa Mungu.

**Faslu ya sita**

Sura hii inaeleza maisha ya Adamu na Hawaa duniani. Maisha yao ni ya shida na taabu. Waliishi katika pango, walidungwa na miba, walipanda miti ambapo baadaye walitunda matunda yake.

Wakati huu hawakuwa wakijua matumizi ya moto na samaki wale waliowakamata waliwala wabichi. Kutokana na uwezo wa Mungu, walikuja kuvumbua moto. Waliweza pia kupanda nafaka na kuzitumia kama chakula. Maisha yalipoendelea, Adamu aliweza kupanua kikataa chake akawa na shamba kubwa. Alipata shida kubeba mizigo na mwishowe aliweza kuwapata wanyama wa nyumbani, mathalan mbuzi, ng'onzi, ng'ombe, punda na hata ngamia. Wanyama hawa walitumika kwa shokoa mbalimbali, fauka ya kuwapatia nyama na maziwa.

Maisha kwa Adamu na Hawaa yaliendelea japo kwa shida na hatimaye Hawaa akapata mimba. Mwanzo Hawaa hakuelewa kilichoendelea katika tumbo lake (ile mimba) na ilimbidi Adamu amkumbushe kuwa alipapia kula Tunda la mti wa kati, alitamani wana na vizazi na kinachokua katika tumbo lake ni zao la wakati ule.

<u>Ubeti wa 446</u>

Watoto ulitamani

Nao ni hao tumboni

Sasa wagutuka nini

Usokaa kutuliya?

Katika ubeti wa 447, sifa kuu ya Hawaa, na wanawake wote wa baadaye inajitokeza kuwa wao ndio wazazi wa watu wote. Hili litakuja kujitokeza wazi tutakapojadili mwanamke kama mzazi.

Katika ubeti huu wa 447, Hawaa asema:-

Hivi kumbe mume wangu

Watoto wa ulimwengu

Watoke tumboni mwangu

Niwe wao mzaliya ?

Adamu anathibitisha haya anaposema katika ubeti wa 450.

Ndiwe mzaa kaumu

Na mimba hii adhimu

Utamzaa Adamu

Mdogo kuinukiya.

Hawaa alipata maumivu wakati wa kuzaa na shida pia kulea. Watoto walizaliwa mapacha umbu na Mungu alimwagiza Adamu kuwa mtu amwoe dada ya ndugu mwenziwe, asimuoe mwenziwe pacha wanaotokeya( ubeti wa 477)

Mtunzi azidi kutueleza kuwa Hawaa alimzaa Habili kisha Kabili. Kabili alikataa dadake pacha aolewe na Habili na mwisho ikawabidi watoe sadaka ili

kuamua aliye makosani. Kabili alitoa sadaka ya nafaka naye Habili ya ng'onzi, lakini sadaka ya Kabili ilikataliwa na ya Habili kukubaliwa.Wivu,tadi na inda zilimpanda Kabili ambaye hatimaye alimuua Habili. Mungu alimwonyesha Kabili jinsi ya kumzika nduguye Habili aliyemuua kupitia mfano wa kunguru waliopigana mmoja kumuua mwenzake kisha kumzika. Kabili vivyo hivyo alimzika nduguye aliyemuua. Kifo cha Habili kinamhuzunisha Hawaa. Alihuzunika zaidi anapofahamu kuwa hata yeye atakufa. Ni peponi tu ambapo Hawaa na Adamu wangeishi milele. Huku duniani atakuwa mzee, nywele ziingie mvi na meno yang'oke. Hawaa anajutia kitendo chake cha awali cha kuasi na katika ubeti 583 na 584 asema:-

Kudumu nilikotaka

Sikupata hakika

Na wana waliosumbuka

Matesoni nimengiya.

Ubeti wa 584

Nilitaka uangavu

Ujuzi na uerevu

Ila sasa upumbavu

Ndio niliopokeya.

Ingawa Hawaa ajutia tendo lake, lakini kitendo cha kula tunda kilikuwa cha '*ujasiri*' mkubwa na inaonyesha kuwa yeye, na wanawake wengine wa

baadaye, ni wapenda maarifa na ujuzi na hii ni sifa kubwa sana ya mwanamke.

Mihimili ya nadharia changamano ya mtafiti ni kuwa sanaa inapaswa kutathminiwa bila ya kuegemea vigezo vingine ,na inatuelekeza kumaizi kuwa matini hii, iliyoegemeza maudhui yake katika Korani tukufu, inamwinua na sikumgandamiza mwanamke .Mwanamke ni shujaa , ni mwangavu na yuapenda ujuzi na maarifa.

Hawaa anakiri dhambi zake na kuomba msamaha kwa Mungu. Beti za 606, 609 zote zinasawiri ombi la Hawaa kwa Mungu; na katika ubeti 610, Hawaa akamilisha maombi ya msamaha kwa Mungu:-

Naomba iwe kabuli

Unisamehe Jalali

Na mtumeyo adili

Utupe njema hidaya.

Mwishowe, Hawaa anarudisha shukrani kwani Adamu anamhakikishia kuwa kupitia Jibrili, Malaika wa Jalali, amesamehewa dhambi zake.

Mtunzi alianza utendi huu kwa kuomba rehema kwa Mungu na kutoka ubeti wa 619 hadi 637, anarudisha shukrani kwake Mungu. Anasifia dini ya Islamu pamoja na kuomba mema yawashukie . Ubeti wa 621

Mungu atuangaze

Memani atuongoze

Topeni tusiteleze

Maovu tukatapiya.

Abdilatif anakamilisha utunzi wake kwa kujitambulisha pamoja na mlezi wake kiushairi ambaye pia ni ndugu yake, Ahmadi Nasiri Juma Bhalo.Kujitambulisha huku ni mtindo wa urasimi ambapo watunzi hujitambulisha katika tungo zao. Anazidi kutueleza ukoo wake na makazi yao.

<u>Ubeti 633</u>

Kwetu sisi kwa yakini

Taweleza mubaini

Tu wa Kuze ya uani

Biladi ya Mambasiya.

Anasisitiza kuwa makazi yale ni ya jamii yao tangu wazee wao.

### 3.1.2 Kijalizo

Mtunzi katika utendi huu amebainisha taswira anuwai za mwanamke. Mwanamke aliumbwa kama msaidizi wa mwanamume, lakini kwa tariki zake anakuwa kizingiti na kusababisha kuanguka kwa Adamu.

Nadharia changamano ya Unisai wa Kidenguzi imemwelekeza mtafiti kutalii maswala muhimu yanayomhusu Hawaa katika utendi wa *Maisha ya Adamu na Hawaa* . Ni bayana kuwa mwanamke ni shujaa , ana 'ujasiri', ni mpenda hekima, na ana uwezo wa kubatilisha matukio ya maisha .

Picha halisi inayojitokeza hapa ni kuwa mwanamke anazo nguvu, japo si za kimwili, za kupata kile anachotaka. Unyonge wa kike huwa ni silaha kali ya kuangusha hata wafalme. Hawaa alijua alichotaka na alikula tunda ili apate hekima. Huu ni 'ujasiri' na ukakamavu alioukosa Adamu, aliyejua matokeo ya kula tunda na aliona ni heri kumkosea Mungu kuliko kumkosea Hawaa.

Hata hvyo,kutenda kosa ambalo umeelezwa kuwa ni kosa na lina madhara si werevu. Mkosaji alidhani 'uasi' wake ungemwongoza kwenye mustakabali wenye kudhibitika.

Mwanamke hapa pia amesawiriwa kama mama wa wote ulimwenguni, ndiye mzaa kaumu duniani, ni mlezi zaidi ya kuwa mama. Ubeti wa 473.

Furaha kajionyesha
Akawa awaamwisha
Usiku kucha akesha
Na wanawe kuwaleya.

Mwanamke ndiye anayeendeleza kizazi . Akiwa kiruka njia, familia hupotea na hata ulezi wa watoto wadogo huathirika . Familia ikisha vurugika, taifa huangamia , kwani familia ndio muundo msingi wa taifa.

Mwanamke pia amesawiriwa kama mwenye mapenzi, mpole na anayeomba toba kwa makosa, labda hili laweza kueleza kwa nini wanawake ndio huwa wengi makanisani: Tazama beti za 606-609.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Ubeti 606

Nimekuasi Rahimu

Amri yako karimu

Ndimi halifu adhimu

Ya ilahi nisikiya.

Ubeti 607

Rabbi ndiwe mwenye nguvu.

Na ndiye murehemevu

Nami ndiye mpumbavu

Kwako wewe natubiya.

Ubeti 608

Nimejitakia zani

Na kumtia kosani

Mtumeyo muumini

Kwa wangu ujahiliya.

Ubeti 609

Nami haya hukweleza

Mola wangu nisikiza

Unisamehe muweza

Madhambi kunifutiya.

Mtunzi ametupa picha ya mwanamke kama mjasiri, mwerevu, mama na mlezi, mpole na aliye na moyo uliojaa mapenzi na toba

## 3.2 MUHTASARI WA PARADISE LOST

### 3.2.0 Utangulizi.

Katika sura hii, mtafiti ametoa muhtasari wa *Paradise Lost kwa* kifupi. Matukio muhimu katika vitabu vyote 12 yamegusiwa. Haya yanagusia matokeo ya utafiti ambayo yameelezwa kinathari. Data hii ilipatikana kwa kusoma miongozo anuwai ya *paradise Lost* na muhtasari wa kila sura katika utendi wenyewe. Aidha nadharia ya Udenguzi ilifaa katika utendi huu kwani muwala wa kazi hii ulijengwa kutokana na mchangamano wa tajriba katika kazi Zilizosomwa na nyingine njeya kazi hizo. Utendi huu uliegemea Biblia katika kueleza kuubwa kwa binadamu wetu wa kwanza.

### 3.2.1 UCHANGANUZI WA PARADISE LOST

**Utangulizi**

Mbinu za utafiti zilihusu usomaji wa kina maktabani. Matokeo ya utafiti yaliongozwa na nadharia ya unisai wa kidenguzi na hili limebainishwa pale inapofaa.

Utendi wa *Paradise Lost* ni mkubwa sana na umeandikwa kwa Kiingereza na una jumla ya vitabu 12. Mtafiti ametoa muhtasari wa kila kitabu ili hadithi yenyewe ieleweke.

**Kitabu cha kwanza** kinatoa muhtasari wa funzo nzima:-Kuasi kwa binadamu na kufukuzwa kutoka alipokuwa amewekwa na Mungu.Tunafafanuliwa chanzo cha uasi na kile kilichofanya binadamu aasi. Kuasi huku kulitokana na ibilisi aliyekuwa katika umbo la nyoka.

Shetani na jeshi lake maluuni walikuwa wamemuasi Mungu, na hivyo kutupwa kutoka mbinguni mpaka katika shimo lisilo na kina.

Shetani na jeshi lake wakiwa pale wanaliwazana katika mwina huu wa giza unaoitwa Vurumai. Katika ziwa hili la moto, Shetani na wafuasi wake wameduwaa, hawajui la kufanya. Wanapozinduka wanaanza kutafakari juu ya hali yao ya baadaye.

Shetani anawaamsha askari jeshi wake na kuwaambia kuwa wanaweza "kukomboa" mbinguni tena. Baraza la Halmashauri la Shetani linatoa hoja anuwai kuhusu huku kupigwa vita, kushindwa na hatimaye kutupwa pale.

Baadhi wanashauri wajizatiti tena na kupiga vita mbinguni. Wengi wanakataa wazo hili kwani bado walikuwa na unyonge mwingi, wengine wanapendekeza wanyenyekee na kutii Mungu, lakini pendekeza hili pia lakataliwa.

Shetani kupitia kwa majemadari wake anapendekeza vita vya kuvizia kwa kulenga viumbe wengine dhaifu kuliko wao, ambao walikuwa wametafsiriwa wataumbwa na Mungu na kuwekwa katika ulimwengu - dunia mpya. Haya yalikuwa kutokana na umbea aliokuwa ameupata huko mbinguni. Mpango huu wa kulipiza kisasi kwa kuvizia viumbe hivi duni vya Mungu unakubaliwa. Hata hivyo, palihitajika mtu wa kujitolea kuabiri safari hii ngumu na ndefu ili kuthibitisha umbea na utabiri huu wa zama. Hakuna kati ya Malaika wa Shetani aliyejitolea na ndiposa Shetani mwenyewe akajitolea. Kitendo hiki cha kishujaa kinashangiliwa na wote na wote wanamkubali Shetani kama kiongozi wao. Makelele ya shangwe yanapigwa na ni hapa ambapo sasa kasri la Shetani linaundwa katika ahera. Hapa wanaanza mashauriano.

Katika **kitabu cha pili**, shetani anaendelea na mashauriano na jeshi lake. Pendekezo la kupiga vita ili kukomboa mbingu lakataliwa kama vile la kunyenyekea lilivyokataliwa.

Pendekezo la tatu la kuvizia linakubaliwa na shetani kujitolea kwa safari hii ndefu ya kwenda kuchuguza viumbe na dunia mpya. Baada ya Halmashauri kukubaliana na mpango huu, malaika hawa wa Ibilisi wanafumukana na kila mmoja kujiendea zake –katika pilkapilka mbalimbali mpaka Shetani atakaporejea.

Shetani anaanza safari yake lakini anakuta milango ya kuzimu imefungwa. Anaketi na kusubiri bawabu anayemfungulia. Milango inapofunguliwa, anaona uwazi uliopo kati ya ahera, na mbingu. Katika milango hii ya ahera, Shetani anakutana na bintiye, Dhambi, na mjukuu wake, Kifo. Dhambi ni binti wa Shetani kwani alizaliwa na Shetani kichwani mwake. Shetani alimnajisi binti huyu Dhambi, na hivyo ni binti na pia mke wake. Kifo ni mwana na pia mjukuu wa Shetani. Shetani anaachana na aila yake hii na akiongozwa na Vurumai, anajitoma kwenye uwazi kati ya ahera na mbingu.

Katika **kitabu cha tatu**, Mungu akiwa ameketi katika kiti chake cha enzi amuona Shetani akipaa kuelekea kwenye ulimwengu ambao ameuumba hivi karibuni. Anamwita mwanaye, aliyeketi upande wake wa kuume, na kumwonyesha Shetani. Wanaona wazi kuwa Shetani atafanikiwa kumrubuni binadamu.

Ingawa binadamu ni kiumbe wa Mungu, Mungu alimuumba siyo kama mwanaserere atakayemtii pasi kufikiri au kuamua, bali kwa kupenda. Ingawa

ni wazi binadamu ataanguka, siyo kwa ubaya au uovu wake kama Shetani, bali kwa hila za Ibilisi. Mungu anatangaza njia za wokovu kwa binadamu. Mwana wa Mungu anampongeza Mungu kwa fadhila zake za wema na wokovu kwa binadamu. Hata hivyo, Mungu anasema wokovu huu hauwezi kutolewa kiholela bila hukumu, kwani binadamu atataka kuwa kama Mungu. Binadamu na vizawa wake lazima wafe. Wokovu wa binadamu waweza kupatikana tu ikiwa patajitokeza mtu achukue dhambi ya binadamu na hivyo kuzuia adhabu ya Mungu.

Mwana wa Mungu anajitolea kama kafara ili kumwokoa binadamu kwa kuchukua lawama yake. Mungu anakubali kujitolea huku na kumpa mwili wa binadamu fauka ya kumtawaza zaidi ya viumbe wote na kulitukuza jina lake. Malaika na viumbe vyote wanamwabudu na kumsujudu, huku wakiimba na kumsifu Mungu na mwana wake.

Wakati huu Shetani aliyekuwa ameelekea ulimwenguni anatua mahali ambapo pana utulivu na ambapo viumbe waliweza kupanda na kushuka mbinguni kwenda ulimwenguni kwa ngazi. Shetani anakutana na malaika Uriel, mwenyezi wa pale. Shetani anajigeuza malaika mdogo anayetaka kutazama na kuajabia viumbe vipya – binadamu - ambao wameumbwa na Mungu. Katika umbo hili, Shetani anaanza matembezi pale.

Katika **kitabu cha nne** shetani sasa amefika Edeni, mahali ambapo sasa anajaribu kutenda kitendo cha kulipiza kisasi kwa Mungu, kwa kumhadaa binadamu. Ana wasiwasi kuhusu uwezo wake wa kutenda hili na hisia nyingi zinamnyonga- anaongopa - ana wivu - ametamauka, lakini hatimaye anajikakamua na kuingia paradiso, akiwa amejawa na uovu.

Akiwa sasa amejigeuza katika umbo la ndege, Shetani anatua juu ya mti wa kati – mti wa maisha –ambao ulikuwa mrefu kuliko miti yote na kuchunguza maeneo na mazunguko yake. Akiwa amejipachika pale, Shetani anawaona Adamu na Hawaa, na anaajabia hali yao ya furaha na kuudhika. Hili lina mkera na anaapa kubuni mbinu awaangushe.

Anawanyemelea wanapozungumza na kufahamu kuwa mti wa kati, mti wa utambuzi, ulikuwa marufuku kwao, ilikuwa muhali kwao kula matunda yake; kwani watakapofanya hivyo, watakufa. Hapa Shetani anapata chambo cha uhani wake kwa binadamu . Shetani anawaacha ili aweze kutafitia zaidi hali yao kwa tariki nyingine.

Malaika Uriel, aliyekuwa akishuka kutoka mbinguni anamuonya malaika Gabriel, aliyekuwa mlinzi wa Paradiso kuwa roho mbaya alikuwa ametoroka kutoka kuzimu na kuingia Paradiso akijifanya mmoja wa Malaika wazuri. Alitambulikana kutokana na jinsi alivyo sasa na alivyokuwa hapo siku za nyuma. Gabrieli anaahidi kuchunguza haya keshoye.

Adamu na Hawaa wanaendelea na mazungumzo yao na baada ya

kuabudu, wanaenda kulala.Gabrieli anaweka walinzi wawalinde wasije wakahasiriwa na pepo mbaya wakiwa wanalala. Hata hivyo katika kukuru kakara zao, wanamkuta Ibilisi akimnongonezea Hawaa akiwa usingizini. Alikuwa akijaribu kumrubuni katika ndoto. Ibilisi anakamatwa na kuletwa mbele ya Gabriel. Anahojiwa, lakini anajibu kwa kiburi katika hali ya kujitetea. Anaponyoka na kutororka/kupaa kutoka Paradiso.

Katika **kitabu cha tano**, asubuhi iliyofuata baada ya kisa cha usiku cha Shetani kumlaghai Hawaa katika ndoto; Hawaa anamsimulia Adamu yote. Adamu hapendezwi na ruwaza hii lakini anamliwaza tu. Wanaanza shughuli zao za kila siku. Siku baada ya maombi na ibada katika kiambo chao, Mungu anamtuma malaika Raphael kumwonya Adamu kuwa kuna pepo mbaya ambaye angekuja kumdanganya. Amweleze bayana pepo huyu ni nani na sababu za kutaka kumrubuni. Amkumbusha Adamu utii – wa kutokula tunda la mti wa utambuzi. Raphael anateremka Paradiso na kukaribishwa vizuri na Adamu. Hawaa anawaandalia maakuli ya matunda,kisha anaenda zake. Ingawa Raphael alimweleza kuwa alikuwa na jambo la kuwaambia, Hawaa anasema amweleze Adamu ambaye angemwarifu baadaye. Raphael anamweleza Adamu adui yao mkubwa, jinsi adui huyo alivyoendeleza vita na uhasama miongoni mwa malaika, jinsi adui huyo alivyoshindwa na hatimaye kutupwa katika lindi la moto.

Katika **kitabu cha sita**; malaika Raphael anaendelea kumweleza Adamu jinsi malaika Mikaeli na Gabriel walivyotumwa kumpiga vita shetani akiwa na malaika walioasi. Shetani alikuwa ameanzisha vita akiwa na wafuasi wake huko mbinguni. Alikuwa ameunda zana za vita lakini hizi, pamoja na askari jeshi wake wote walishindwa. Vita kati ya malaika Mikaeli pamoja na Gabriel dhidi ya Shetani na askari wake viliendelea kwa siku mbili. Siku ya tatu, Mungu alimtuma mwanaye, akiwa na utukufu aliomtukuza - utukufu wa ushindi. Malaika wa Mungu walimpisha na kama ngurumo akashuka kati ya adui na kuwafuata hadi ukingo wa mbinguni. Mwanya ulifunguka pale na Shetani na jeshi lake walijitupa katika lindi hili lisilo na kina, lindi la moto, ambalo walikuwa wameandaliwa. Baada ya ushindi huu, Mwokozi anarudi kwa baba yake.

**Kitabu cha saba** ni mazungumzo kati ya Adamu na malaika Raphael. Hapa Adamu anamuuliza Raphael jinsi ulimwengu ulivyoumbwa. Anaelezwa kuwa baada ya Shetani na malaika wake kufukuzwa kutoka mbinguni, Mungu alionelea ni bora aumbe ulimwengu mwingine ambako viumbe vyake vingeishi. Akiwa na mwanaye na utukufu wote wa malaika, Mungu aliumba ulimwengu kwa siku sita. Kulikuwa na sherehe baada ya uumbaji huu na malaika wakarudi mbinguni.

Mazungumzo haya juu ya kuumbwa kwa ulimwengu, kuumbwa kwa Adamu na Hawaa na vyote vilivyomo ulimwenguni yanaendelea katika **kitabu cha**

**nane**. Hapa maswali ya Adamu kuhusu sayari na anga yanajibiwa. Huku akimdadisi Raphael zaidi, Adamu anaeleza yote anayoweza kukumbuka tangu aumbwe na kuwekwa kwake Paradiso. Mazungumzo yake na Mungu kuhusu upweke wake, jinsi alivyokutana na Hawaa na nikahi yao, mazungumzo na malaika hapo baadaye na hatimaye Raphael anarudi mbinguni.

Katika **kitabu cha tisa**, shetani, baada ya kuzunguka ulimwenguni kwa ujanjo mkubwa anarudi Paradiso usiku kama ukungu. Anaingilia nyoka akiwa amelala. Machweo, Adamu na Hawaa wanaendelea na shughuli zao za kila siku. Hawaa anaonelea ni bora kila mtu aendelee na shughuli zake kipekee kwani wakiwa pamoja kazi yaenda polepole. Adamu katu hakutaka watengane kwani alikuwa ameshaonywa kuwa Ibilisi angewaghilibu. Kuhusu kutekwa bakunja, Hawaa anasisitiza uhuru wake na kuwa alikuwa na akili ya kujiamulia na uwezo wa kujizuia dhidi ya ghilibu zozote.

Kwa shingo upande, Adamu anakubali pendekezo la Hawaa. Hawaa anajiendea zake ambapo Ibilisi anampata akiwa yu pekee.

Kwa hila nyingi, Ibilisi akiwa mfano wa nyoka anamlaghai Hawaa; jinsi alivyoumbika na alivyo mzuri kushinda viumbe vyote. Hawaa , akiwa na shauku anamuuliza nyoka jinsi anavyoweza kuongea kama binadamu. Nyoko

(Ibilisi) anamwambia ni kwa kula tunda fulani la mti. Tunda ambalo hata wao (Adamu na Hawaa) wakila watajua mema na mabaya. Hawaa anaomba aonyeshwe mti unaozaa matunda hayo. Akiwa na ushupavu mwingi, Ibilisi anamwelekeza Hawaa kwenye mti wa uzima. Kwa hila nyingi, Hawaa anashawishika na kula matunda ya mti wa kati. Wakati huu wote, Adamu anayedhani Hawaa amepotea, anamkuta kwenye ule mti wa kati. Hawaa anamshawishi Adamu ale pia tunda la mti ule wa uzima.

Ni baada ya kitendo hiki ambapo wanajiona wa uchi na wanaanza kulaumiana kwa kosa lao.

Katika **kitabu cha 11**, mwana wa Mungu anamweleza Mungu juu ya maombi ya wazazi wetu wa kwanza ambao sasa wametubu. Anajitolea kuwa kivuko kati ya Mungu na binadamu. Mungu anakubali ombi la msamaha wa wavyele wetu hawa, lakini anaeleza katu hawawezi kuendelea kuishi Paradiso. Ili kutekeleza azimio hili, Mungu anamtuma malaika Mikaili akiwa na makerubi awatimue Adamu na Hawaa toka paradise

.

Kitabu cha 10 mshororo wa 99:-

Mikaili

Nataka uwe kiongozi jemadari

Chukua toka miongoni mwa jeshi

Askari uonao wazuri

Ili kuzuia waovu

Kwa niaba ya binadamu

Wanaoweza kuingia paradiso

Hivyo kuzua tandabelua mpya.

Harakisha

Toka paradiso ya Mungu

Bila huruma

Uwatoe binadamu wenye dhambi

Toka mahali pale patakatifu.

Kabla ya kuwatokomeza, Mikaili anaambiwa amweleze Adamu mambo yatakayojiri usoni. Mshororo wa 113

.... mfunulie Adamu

Mambo yatakayojiri

... wafukuze,

Japo wana huzuni,

lakini waende kwa amani.

Mikaili anaamrishwa baada ya kuwafukuza binadamu aweke askari watakaolinda lango la paradiso ili binadamu asiweze kurudi tena.

Mikaili anashuka toka mbinguni hadi paradiso na hapo Adamu anahisi jambo baya liko karibu kutendeka. Anamaizi kufika kwa Mikaili na anaenda kumlaki. Mikaili anamweleza Adamu hukumu ya Mungu.

Hawaa aliyekuwa ameotea karibu, lakini hakuonekana alisikia yote na kuomboleza mno. Adamu anasihi wasifukuzwe japo anatii amri ya Mungu ya kutokomea toka paradiso.

Malaika anamwongoza Adamu kwenye mlima na hapo anampa ufunuo wa yatakayojiri wakati wa gharika. Mshororo wa 840:

> Akaangalia na kuona
>
> Safina ikielea juu ya gharika.

Ufunuo huu ulimpa Adamu nafuu katika hali yao ya sasa- kuwa kulikuwa na tumaini katika maisha.

Katika **kitabu cha 12** na cha mwisho, malaika Mikaili, kutoka maelezo ya safina na gharika, anamueleza Adamu juu ya Ibrahimu.

Hatua kwa hatua, anamweleza juu ya mwokozi atakayezaliwa na ambaye waliahidiwa baada ya kuanguka katika paradiso. Anaelezwa jinsi mwokozi huyu atakavyokuja katika mwili wa binadamu, kufa na kufufuka kwake na kisha kurudi mbinguni tena kwa baba yake. Mwokozi huyu ataacha wafuasi watakaounda kanisa na kuendelea kupigana na Shetani hadi kuja kwake mara ya pili.

Adamu akiwa ameridhika na kufarijika na mahusiano aliyoonyeshwa, pamoja



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

na ahadi alizopewa, anatoka mlimani akiwa na malaika Mikaili. Anaenda na kumwamsha Hawaa, ambaye amekuwa katika usingizi wenye utulivu, aman na utoshelevu. Mikaili anawashika mikono, kila mmoja upande wake, na kuwaongoza nje ya paradiso.

Upanga wa moto uliogeuka huku na huko uliwekwa kwenye lango la Edeni, pamoja na Makerubi ili kumzuia binadamu asirudi humo asilani.

### 3.2.2 KIISHILIO

Mtafiti alitumia njia ya usomaji wa vitabu, makabrasha,machapisho, majarida na kadhalika kukusanya data. Aliweza kudondoa mambo muhimu yaliyohusiana na utafiti wake katika usomaji huu. Amerejelea tendi mbili za *Paradise Lost* ya John Milton na *Utendi wa Maisha ya Adamu na_Hawaa* wa Abdilatif Abdala. Fauka ya vitabu hivi viwili, mtafiti amerejelea vitabu vingine vinavyoshughulikia au kujadili masuala ya kijinsia. Ameegemea vitabu vitakatifu - Biblia na Korani. Katika utafiti huu,mtafiti aliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- Mwanamke anazo nguvu nyingi katika unyonge wake.
- Kinyume na inavyochukuliwa na wengi,dini haimgandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi.
- Kuendelea ama kufaulu kwa maamuzi, mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke.

Dini ni majawapo ya asasi zinazodaiwa kuwa zinamdunisha mwanamke. Katika tendi mbili mtafiti alizorejelea,mwanamke amesawiriwa akiwa bora kuliko mwanamume, kwani mwanamume anaona ni heri amkosee Mungu kuliko kumkosa mwanamke. Kwa kudengua matini hizi, ni bayana kuwa dini haimbagui mwanamke , bali inamwinua na kumpa hadhi - inamchukua kama binadamu bora kushinda mwanamume.

Akizungumza juu ya nafasi ya dini katika maisha ya wanawake, Andersen (1997: 223) katika *Thinking About Women* asema:-

> ... Kwa miaka mingi, dini imekuwa mihimili mikubwa katika mitazamo ya kifeministi na mitazamo mingine ya kisiasa na kijamii inayohusika na ukombozi wa binadamu. Hili linajitokeza bayana katika jamii ya Afrika- Amerika (African -American Community) ambapo dini imekuwa ala muhimu ya kuleta mabadiliko ya kijamii . Jukumu la mwanamke katika kanisa kunampa Mwafrika - Mwamerika nafasi ya uongozi, elimu na kukuza vipawa vyake vya usimamizi. Aidha , imani za kidini kwa jamii nyeusi zimeundwa chini ya mizizi shakiki ya imani katika sheria, haki na usawa. (T.M)

Dondoo hili latilia nguvu dhana kuwa dini ni kiegemeo kikubwa kwa mwanamke, na wala si kisiki au kizingiti kwa uhuru wa mwanamke .

Katika nadharia tete, mtafiti alitaka kubainisha kuwa kuendelea au kufaulu kwa maamuzi , mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke. Juhudi za kumkomboa mwanamke kutokana na pingu za mila,dini, na utamaduni zitafaulu tu pale ambapo wanawake watakuwa washiriki na watendaji zaidi kuliko watazamaji kwani adui mkubwa wa mwanamke si mwanamume, si dini, si ndoa, si utamaduni , ni mwanamke mwenzake. Hadithi ya msanii Rayya Timammy (Uteuzi wa Moyoni) katika *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) imeorodhesha vikwazo na mateso anayokumbana nayo mwanamke. Kikwazo kikubwa katika Ukombozi wa mwanamke ni mwanamke mwenzake.Mwanamke hajakubali kuwa ana uwezo.Wanawake wamejifungia katika ngome - ya nafsi zao. Hawajapevuka kuona kuwa wanao uwezo. Msanii huyu anatoa mfano wa Zena anayeteswa na mumewe, lakini aelekezwa lawama zote. Mamake Bi Saidi anamlaumu Zena kwa matatizo yanayompata, hamlaumu Ali mumewe, ingawa Ali ndiye mtesi. Zena anadhihakiwa na wanawake wenziwe anapotaka kupigania ubunge.

Z.Burhani (1981) katika riwaya ya *Mali ya Maskini* anasema kuwa uganga wa mwanamke ni mmoja tu...Kujiamini tu kuwa yeye ni mwanamke wa kutosha.Maana hapo hata yule mbaya huonekana mzuri. Imani yake ndiyo inayompa nuru.

Tomaseveski (1995) Katika_*Women and Human rights*: asema:-

> Sisi wanawake hatujui mengi kuhusu historia na utambulisho wetu. Hata sisi wenyewe hatujijui; na tumenyimwa njia za kujijua. Huwa tunakubali visa na uwongo tunaoambiwa kutuhusu hata kama unakizana na hisia zetu. Tunazuiwa kujiona vizuri. Tunatumia wakati mwingi kuangalia wengine hivyo tunabakia katika vivuli vyao. Tunaambiwa jinsi tunavyoonekana na wengine na hii inakuwa hali tosha ya sisi kuishi.(T.M)

Kwa kweli wanawake huishi katika hali ya kuwaangalia wanawake wengine - libasi,watoto, mitindo ya nywele, maendeleo yoyote kwa jumla na kadhalika. Ikiwa haya ni kushinda yake , hii husababisha kijicho na umbea.Lakini akiona yu bora , hili humtia kiburi na majivuno .Wivu huu nadhani ndio huwafanya wanawake kuingilia maisha ya wengine.

Monica Lewnsky, alikubali kutongozwa na Bill Clinton, akijua wazi huku ni kumhujumu Hilarry Clinton, mkewe. Mke wa Sunkuli alikubali kumtetea mumewe, akijua wazi hili lingebatilisha ushahidi dhidi ya Florence Nangini Mpayei, banati aliyepachikwa mimba na Sunkuli- kwa kubakwa, akiwa na

umri wa miaka 14 tu. Je, adui mkubwa wa mwanamke si mwanamke mwenzake?

Kongamano la kwanza la kitaifa la wanawake nchini Kenya lilifanyika katika jumba la Kimataifa la Kenyatta tarehe 22/02/1992. Hapa wanawake kutoka kila nyanja ya maisha walihudhuria –Wakulima wadogo, wafanyikazi wa kijamii, wachuuzi, wahadhiri wa vyuo vikuu, watarazaki na wafanyi biashara wakubwa , wafanyi kazi wa serikali na walionuia kujitupa ulingoni mwa siasa ; na wote wakakubaliana kuwa kuna umuhimu mkubwa wa wanawake katika nyanja zote za maendeleo nchini. Mchango wa wanawake katika sekta za kilimo, uchumi, umma, mashirika ya kiserikali na yale yasiyo ya serikali ulipongezwa; japo kulikuwa na shaka kuhusu kudunishwa kwa jukumu la mwanamke na taswira yake katika jamii. Hatimaye ilikubaliwa kuwa wanawake walio nusu ya Wakenya wote walikuwa kundi kubwa kiasi kwamba wangeweza kubadilisha hatima ya nchi: Kura ndiyo iliyokuwa silaha ambayo wanawake wangeitumia kwa maslahi yao na ya taifa kwa jumla. Kwayo, wanawake wangeweza kupata uwakilishi katika sekta muhimu na haswa katika mashirika yanayotunga na kupitisha sheria (Tomaseveski. K 1995).

Ingawa takriban miaka 15 imeyoyoma, mpaka sasa ni wanawake wachache wanaochaguliwa katika uchaguzi mkuu kama wabunge. Kuna wanawake

wasomi na viongozi bora wanaosimama, lakini wanawake wenzao hawawachagui. Tunakubaliana kwa kiwango fulani na Maillu (1988) anaposema kuwa shida ya mwanamke ni kwamba ni kama hakijui kile anachokitaka, lakini anatarajia aeleweke.

Maoni ya Tomaseveski (1995) yanafanana na ya Saadawi (1980) anaposema:

> Tumegundua kwamba sisi wanawake katika nchi za Kiarabu bado tu watumwa; bado tumegandamizwa. Siyo kwa sababu tu wa mashariki, siyo kwa sababu sisi tu Waarabu au wanachama wa mashirika ya Kiislamu, lakini kwa sababu ya mfumo wa kuumeni ambao umetawala ulimwenguni kwa miaka na mikaka. Njia pekee ya kuwa huru ni kuondoa mfumo huu. Uhuru wa wanawake utakuja kupatikana wakati wanawake watakapoungana katika makundi ya kisiasa yenye nguvu, uwezo na elimumwendo wa kuwakilisha nusu ya jamii.

Kuungana kwa wanawake bila kuwa na wivu, kijicho au bezo ndiko kutakakoleta mageuzi ya kisiasa na hivyo uhuru kamili wa mwanamke. Mfano bora wa muungano huu unapatikana katika Biblia, kitabu cha Ruthu. Hapa tunamwona Naomi aliyefiwa na mumewe Elimeleki na wanawe wawili Meloni na Kilioni, akiwashauri wakaza wanawe warudi kwa mama zao Moabu

kwani yeye mwenyewe alikuwa anarudi Bethlehemu. Mkazamwana mmoja, Orpa alikubali, lakini yule mwingine, Ruth , alikataa. Alitaka kuungana na Naomi kwa vyovyote vile (Kitabu cha Ruthu 1:16-18). Wanawake hawa wawili, Naomi na Ruthu ni wajane, hawana watoto, wana ulitima na wametengana na aila yao, lakini muungano wao unaleta ufanisi kwa wote wawili. Kwa ushirikiano na kuungana, Ruthu alifanikiwa kuolewa na Boazi, ndugu yake Elimeleki.Ruthu alipata mtoto Obedi, aliyelelewa na Naomi. Obedi alimzaa Yese, naye Yese akamzaa Daudi, na kutoka ukoo wa Yese ,Yesu Kristo akazaliwa (Kitabu cha Ruthu 4:16-17).

Ukombozi wa walimwengu kutokana na dhambi ya kwanza ya Adamu na Hawaa ulipatikana kupitia kwa Masiha Yesu Kristo.Masiha huyu ni kizazi cha ukoo wa Daudi, aliyezaliwa kutokana na muungano wa Naomi na Ruthu. Ushirikiano na muungano wa wanawake ndio utakaozaa 'mwokozi' wa kweli katika maisha yao.Muungano wa wanawake umeidhinishwa na Biblia na hii inasadifu mihimili ya utfiti kuwa : Dini haimbagui mwanamke,na kufaulu au kuendelea kwa maamuzi , mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke.

Betty Friedan katika *The Feminine Mystique* ana mawazo kama yale ya Tomaseveski. Anasema kuwa maisha ya mwanamke, kwa kiasi kikubwa, ni mzingile siyo tu kwa wanaume, bali kwa wanawake wenyewe. Mwandishi

huyu anasema kuwa kutoyaelewa maisha yao kumebakia msingi mkubwa wa hali ya maisha ya wanawake kwa jumla.

Ndungo (1985) anasisitiza kuwa wanawake kama wanadamu wana uwezo wa kubadilisha mazingira na historia yao. Katika mabadiliko, matokeo yatategemea juhudi na mwelekeo wa wanawake wenyewe.

## SURA YA NNE

# 4.0. MTAZAMO MPYA WA USAWIRI WA MWANAMKE

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii usawiri mpya wa mwanamke umechunguzwa. Ni bayana kuwa katika muktadha wa kidini mwanamke amechukua nafasi kubwa katika mahusiano yake na Shetani, Adamu na Mungu. Haya yamejiri bayana katika *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* na *Paradise Lost.*

Nadharia ya udenguzi inaendeleza kuwa matini ni chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha. Mhimili mwingine wa nadharia hii ni kuwa sanaa inajitegemea na inapaswa kutathminiwa bila ya kuegemea vigezo vingine. Nadharia hii ilioanishwa na nadharia ya unisai na hivyo kuwezesha kumsawiri mwanamke upya.

Nadharia ya unisai/ufeministi hujaribu kueleza hali inayomkumba mwanamke ili aweze kueleweka na wengi. Hujaribu kuinua hadhi ya wanawake na kuendeleza na kukuza hisia za umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa.

Nadharia hizi mbili, yaani Unisai wa Kidenguzi kwa pamoja, zimetoa picha ya mwanamke kama mwenye busara, mwenye nguvu, shujaa, mpatanishi na muamuzi wa masuala muhimu maishani.Hali hizi zinaweza kuthibitishwa kama ifuatavyo.

## 4.2 MWANAMKE KAMA MWENYE HEKIMA.

Mtu mwenye hekima huwa na akili au busara. Hiki ni kipawa ambacho si kila mtu huwa nacho. Kutokana na *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* na utendi wa *Paradise Lost,* tunaona mwanamke akichukua hatua kubwa katika maisha yake, hatua ya kutaka kujua, kujua kwa nini mti ule wa kati ukaharamishwa na Mungu.

Hawaa ni mweledi kuliko Adamu, anaelewa kile ambacho Adamu hakijui. Yuaelewa kuwa mti wa kati una matunda matamu na ya kusisimua zaidi kuliko matunda mengine Paradiso. Ubeti wa 317 katika utendi wa *Maisha ya Adamu na Hawaa* mtunzi asema:-

Akaliona ni zuri
Ja siagi tiritiri
Jepesi kama Hariri
Tunda lilivyolegeya.

Na katika ubeti wa 331, Hawaa yuasisitiza:-

Tunda hili muadhamu
Ni la mti wa kudumu
Wa maisha ya dawamu
Kwa ambaye hujiliya.

Matunda ya mti wa katikati yanazua hekima, na kwa hekima uwezo wa kupambanua mema na mabaya. Hawaa alikuwa mwepesi wa fikra na hisi kutambua kuwa onyo la Mungu kuwa wasikaribie matunda ya mti ule kulifichika kusudio fulani. Kulikuwa na jaribio la kuficha ukweli fulani, na uongo kuwa kama mikono yao ingenyoshwa matawini na meno yao kuuma lile tunda jororo ja siagi tiritiri, fikra na akili zao zingefunguka na waweze kumaizi kati ya mema na mawi , kutoka wakati huo, wangekuwa kiwango kimoja na muumba wao. Binadamu, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu angekuwa kama Mungu (Saadawi N.E 1980).

Hawaa alimshinda muumba (Mungu) alipomshawishi Adamu amtii yeye kuliko kumtii Mungu , na hii ni ithibati tosha kuwa nwanamke ana nguvu nyingi na vivyo hivyo,dini haigandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi .Hii inashadidi nadharia tete za mtafiti.

Ni bayana kuwa kula tunda kuliwaletea hekima.Katika Biblia, (Mwanzo 3:22 ) tunapata ushahidi wa hili:

> Bwana Mungu akasema, basi huyu mtu
> amekuwa kama mmoja wetu,
> kwa kujua mema na mabaya,
> na sasa asije akanyosha mkono wake
> akatwaa matunda ya mti wa uzima,
> akala akaishi milele.

Katika *Paradise Lost,* tunaona Ibilisi akimwambia Hawaa kuwa kula kwa matunda ya mti wa kati hakutaleta kifo kama walivyoambiwa na Mungu, bali kutamfanya kupambanua mema na mabaya. Hali hii ya kutaka kujua inaonyesha ushujaa na ukakamavu wa hali ya juu na ni nguvu alizo nazo mwanamke. Kitendo cha Hawaa cha kula tunda ni cha ushujaa kinyume na cha Adamu. Adamu alijua wazi amri ya Mungu lakini akaonelea ni vyema amkosee Mungu kuliko kumpoteza Hawaa. Adamu alilila tunda, si ajue mema na mabaya, bali amridhishe mwanamke. Walilotenda na yaliyojiri baadaye yalitegemea uamuzi wa mwanamke na hili ni dhana ghadi ya maisha ya wanadamu wote. Hii inadhiirisha nadharia tete ya mtafiti kuwa kuendelea au kufaulu kwa maamuzi, mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke. Kitendo cha mwanamume cha kula tunda ili amfurahishe mwanamke kinamsawiri kama mjinga na asiye na msimamo mbele ya mwanamke, na hii ni dhana ghadi ya wanaume wote wa baadaye.

Katika Biblia, tunasawiriwa mwanamke Sarai kama mwenye hekima na busara. Katika kitabu cha Mwanzo sura ya 16, tunaelezewa kisa ambapo Sarai, baada ya kutambua hawezi kuzaa, alimchukua mjakazi wake, Hajiri na kumpa Abramu awe mkewe. Hajiri alimzalia Abramu mwana wa kiume naye akamwita Ishmaeli.

Tukiendelea mbele Mwanzo 20, tunaona kuwa hatimaye naye Sara aliweza kupata mtoto Isaka japo alikuwa mzee. Sara aling'amua ukinzano utakaokuwepo iwapo vijana hawa wawili, Isaka na Ishmaeli wangeishi pamoja. Mwanzo 21:9-10.

> Sara akamwona yule mwana wa Hajiri Mmisri,
> ambaye alimzalia Ibrahimu, anafanya dhihaka.
> Kwa hivyo akamwambia Ibrahimu.
> Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe,
> maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na
> mwanangu, Isaka.

Katika Biblia Mwanzo 21:14, tunaona Ibrahimu akitimiza wajibu wa mkewe. Kitendo cha Sara kilionyesha hekima na busara, kwani fahali wawili hawakai zizi moja ila mmoja awe amehasiwa. Vilevile kitendo hiki ni mwangwi wa kitendo cha Hawaa - cha kumfanya mwanamume atende kile mwanamke anachotaka. Kama vile Adamu alvyomtii mkewe Hawaa na kula tunda katavu, Ibrahimu anamtii mkewe Sara ! Aambiwa achukue mjakazi, amfanye mkewe na akisha kuzaa , yu aambiwa amfukuze na anafanya vivyo hivyo. Huu ni ujinga na upumbavu wa mwanamume.Kwa kumwonyesha mwanamke akiwa na hekima zaidi ya mwanamume , dini hapa inamwinua mwanamke na kumpa hadhi na hii inasadifu nadharia tete ya mtafiti

Pierre Grelot (1964) *Man and Wife in Scripture* , asema kuwa mwanamume alipewa mwanamke awe kichwa chake , kiongozi wake, aliumbwa mbele ya mwanamke, lakini akashawishika, akamfuata Hawaa katika njia ambazo Hawaa alikuwa amechagua kwa hiari. Kadhia hizi zote zinatoa ithibati nadharia ya mtafiti kuwa ;

[1]Maswala yanayomhusu mwanamke katika matini yanaweza kuelezeka bayana bika kurejelea muktadha.

[2]Matini ya Unisai wa Kidenguzi inajitegemea na inapaswa kutathminiwa bila ya kurejelea vigezo vingine.

[3]Unisai wa Kidenguzi ni uwazaji au mawazo ya akili bali sio kitu kinachoweza kuguswa au kuonekana .

[4]Matini ya Unisai wa Kidenguzi haijifungi kwenye kaida za uhalisi wa mandhari au jumuiya yake.

## 4.3 MWANAMKE KAMA MWENYE NGUVU

Kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu, nguvu ni uwezo wa kufanya jambo, madaraka. Fasili hii ndiyo mtafiti anarejelea katika kazi hii. Nguvu za kutenda au kufanya mambo zategemea mambo mengi. Kuna nguvu za kimwili, yaani watu wa miraba minne; watu wa aina hii kama vile Samsoni katika Biblia, huweza, kwa kutumia nguvu za misuli, kufanya kazi ngumu.

Kuna watu wenye nguvu za kiroho ambao waweza kuomba jambo likatendeka au kuondoka. Kuna watu wenye nguvu za usemi ambao waweza kuwachochea watu wakagoma, wakapigana, wakalia au wakacheka kipumbavu na kadhalika.

Kuna watu wenye nguvu za akili kiasi kwamba watafikiri majibu ya shida na matatizo na kufikiria njia bora za kuendeleza maisha kila uchao. Baadhi ya watu wamepewa nguvu za aina yote.

Kwa kupitia tendi hizi mbili- *Paradise Lost* na Utendi wa *Maisha ya Adamu na Hawaa*, mtafiti amebaini kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu, si mdhaifu. Nguvu zake si za kimwili , bali ni za ufasaha wa kusema na kushawishi.Katika tendi zote mbili, tunaona Hawaa akimrai Adamu ale tunda la mti walioharamishwa. Hawaa hakutumia kingine ila ulimi wake na viambata vya hisi ya mwili kumfanya Adamu atende lile alilotaka. Hiki ni kiakis cha wanawake wote wa baadaye na usadifu wa madhumuni ya utafiti.

Katika ubeti wa 347 katika *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa*, Hawaa amwambia Adamu:-

> Kama wanipenda kweli
> Adamu ungekubali
> Ukalila tunda hili
> Moyo wangu hatuliya.

Hapo bila shaka Hawaa ashawishi kwa maneno, maneno matamu yaliyotumiwa ndani ya hisi fulani ambayo inaleta nguvu. Adamu anapokosa kuingia katika mtengo huu,Hawaa anatumia nguvu zingine - nguvu za machozi. Katika ubeti wa 335 mtunzi atueleza.:

Kunena maneno hayo
Akachafukwa na moyo
Akaangua kiliyo
Bibi Hawaa kuliya.

Katika ubeti wa 358, Hawaa anachanganya kalima na kulia , nguvu za aina zote mbili -kupata kile anachotaka. Anamwambia Adamu:-

Kulia mimi sipendi
Ni ajili hunipendi
Nitakalo hulitendi
Ndipo mimi nikaliya.

Chacha. (1980), katika tasnifu yake asema;

Silaha kubwa ya mwanamke ni machozi.
Moyo wa mwanamume hauna nguvu mbele
ya machozi na macho ya kulegea ya mwanamke.

Kulia huonekana kama dalili ya udhaifu, lakini chini ya 'udhaifu' huu huwa kuna mizizi imara inayoshikilia jambo fulani. Jambo hili huwa ni kile mwanamke

anachodhamiria kutekeleza. Hili linaunga mkono nadharia ya mtafiti kuwa mwanamke anazo nguvu nyingi katika udhaifu wake.

Kitabu cha 9 cha *Paradise Lost* kinatuangazia nguvu hizi za mwanamke ambazo zinajitokeza katika maneno:

> ...Kama wanipenda... ungenitimizia haja yangu....

Maneno haya 'kama wanipenda' yanayotumiwa na wanawake kwa waume au wapenzi wao, hufanikisha au kuangamiza mambo mengi maishani. 'Kama wanipenda ungeniambia siri za nguvu zako'-Delila alimsihi Samsoni. Madhara ya maneno haya tunayajua. Maneno haya, yakitiliwa nguvu na kilio huweza kuwa silaha kali ya kuangusha hata wafalme. Matini hizi basi zinatuwezesha kumsawiri mwanamke upya - Ana hekima na ni mwenye nguvu.

Abdilatif Abdalla na John Milton, japo ni wa dini tofauti, japo waliishi nyakati mbalimbali na sehemu tofauti, wote katika tendi tulizotaja wanaibuka na wazo moja: Hawaa aliweza kupata kile alichokitaka. Kitendo hiki cha Hawaa ni kiakisi cha wanawake wote ulimwenguni kuwa wana nguvu katika 'unyonge'wao na wanaposhikilia kitu, lazima wakipate.

Hawaa aliweza kumfanya Adamu ale tunda katavu,Delila alifaulu kumshawishi Samsoni atoboe siri za nguvu zake na Sara alimshurutisha Ibrahimu kumfukuza Hajiri na mwanawe.

Saadawi (1980) Katika *The Hidden Face of Eve*. Anatueleza juu ya Aisha, mke mchanga kabisa wa Mtume Mohammed. Asema:-

> Aisha alikuwa na msimamo thabiti nyakati zile. Alitwaa hekima na busara nyingi ambazo wakati mwingi zilitoshana na za Mtume wa Allah.. (T.M)

Saadawi azidi kutueleza kuwa Aisha, fauka ya nguvu za busara, alikuwa pia na nguvu za kimwili :

> .. Aisha alipigana, katika mapambano na kondo mbalimbali. Alihusika sana na siasa, na shughuli za utamaduni na elimu, alifikisha umri wa miaka 18 baada ya kifo cha Mohamad. (T.M)

Kama tulivyotangulia kusema , busara na hekima ni nguvu ambazo huleta mabadiliko na mageuzi na mwanamke anazo.Koran, iliyoegemewa na mtunzi kuandika *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* , inatusaidia kumsawiri mwanamke upya - kama mwenye nguvu na hekima . Aidha nadharia tete ya mtafiti kuwa dini haimgandamizi mwanamke inapiga ndip Aisha ni mwanamke mwenye hekima ,ana busara ,ni shujaa na anashiriki katika shughuli mbalimbali muhimu za maisha.

Milton (1671) katika *Samson Agonistes* anatueleza kisa cha Delila. Samson alikuwa mnadhiri wa Mungu na alipewa nguvu nyingi. Siri yake kubwa ilikuw

kwamba hakuwahi kunyolewa hata siku moja tangu azaliwe. Alikuwa na nguvu nyingi na aliua wanyama mbuaji kama simba kwa mikono yake, pamoja na majeshi mengi ya maadui. Mbinu nyingi ziliwekwa na Wapelestina ili kugundua siri ya nguvu zake lakini hizi zote ziliambulia patupu.

Delila, kwa kutumia nguvu za kike, *Maneno matamu na machozi*, aliweza kumdengua Samsoni na hivyo kummaliza.

Dini haimgandamizi mwanamke, kinyume na vile maulama wengi wanavyodai, bali imempa nguvu na uwezo. Haya tumekwisha thibitisha kwa kutoa mfano wa Aisha , na kisa cha Adamu na Hawaa, Ibrahimu na Sara, na sasa kupitia kwa Samson na Delila.

Kama mama yetu wa kwanza Hawaa, Delila alitumia nguvu za kike kupata kile alichotaka. Katika Biblia, kitabu cha Waamuzi 14:16-17, twaambiwa;

> Basi mkewe Samsoni akalia mbele yake,
>
> akasema, wewe wanichukia tu, wala hunipendi....

Machozi na maneno haya hatimaye yalimfanya Samsoni kutoa jibu la kitendawili alichokuwa amewategea wakwe zake.Katika kitabu cha Waamuzi sura ya 16, kisa cha Samsoni na Delila kama alivyokisawiri Milton (1671) katika *Samson Agonistes* kinaelezwa bayana. Kwa kutumia silaha kali ya mwanamke, unyenyekevu, maneno matamu na machozi, Delila anaonyesha nguvu za mwanamke kwani anafaulu kumshawishi Samsoni atoboe siri zake.

Kitabu cha Waamuzi 16:15-17:

> Mwanamke akamwambia,wawezaje kusema.
> Nakupenda na moyo wako, haupo pamoja nami?
> Umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia
> asili ya nguvu zako nyingi... Ndipo alipomwambia
> yote yaliyokuwa moyoni mwake, akamwambia.
> Wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe;
> maana mimi nimekuwa mnadhiri wa Mungu,
> tangu tumboni mwa mama yangu; nikinyolewa,
> ndipo nguvu zangu zitanitoka, nami nitakuwa dhaifu,
> nitakuwa kama wanadamu wenzangu.

Ni kweli kuwa Samsoni *alikuwa na nguvu nyingi lakini katika nguvu zile kulikuwa na unyonge. Delila alikuwa na unyonge wa kike, lakini katika unyonge ule kulikuwa na nguvu nyingi*.... Ni kweli kuna nguvu katika unyonge na unyonge katika nguvu. Biblia iliyorejelewa kuandika *P.L* inatusawiria mwanamke upya kama mwenye nguvu katika unyonge wake, na mwenye hekima.Haya yote yanasadifu nadharia tete ya mtafiti na kuidhinisha madhumuni ya uafiti.

Chacha(1980) anatubainishia nguvu hizi za kike anaposema:

> ... Miji inapoanguka au nchi zinazopinduliwa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kwa sababu mume au Rais, badala ya kuwa

mwangalifu, anaridhia mwanamke yale anayotaka

baada ya kuwa ameonyeshwa machozi kidogo.

Ndiyo, machozi ya mwanamke ni silaha hatari anayoitumia kufauilisha anachokitaka au kuangusha asichokitaka.

Katika Biblia, kitabu cha Wimbo Ulio Bora (2:16),mwandishi asema:

Mpendwa wangu ni wangu,

Na mimi ni wake…

Hatuoni mwanamke akidunishwa hapa. Twaona picha ya wapenzi wawili walio kufu. Hivyo dini haimdunishi mwanamke.

Katika kitabu hicho cha Wimbo Ulio Bora( 8:10), mwandishi aongeza:

Mimi nalikuwa ukuta,

Na maziwa yangu kama minara

Ndipo nikawa machoni pake

Kama mtu aliyeipata amani.

Kulinganishwa kwa maziwa ya mwanamke na mnara kunaashiria nguvu za kike.Ukuta pia ni kiashiria cha nguvu na uthibati.

Kulingana na Pardes (1993:118), kitabu cha Wimbo Ulio Bora kilikusudiwa kukosoa dhana inayosawiriwa katika kitabu cha Mwanzo cha Biblia kuwa mwanamume ni bora kuliko mwanamke

'… na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala..'

ndiyo hukumu mwanamke aliyopewa katika kitabu cha Mwanzo 3:16.

Kinyume na hili, katika Wimbo Ulio Bora mwandishi anarudia tena na tena

'Mpendwa wangu ni wangu

na mimi ni wake'

Hii haionyeshi kungandamizwa, bali hali ya usawa. Nadharia tete ya mtafiti kuwa dini haimgandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi inapiga ndipo.

## 4.4 MWANAMKE KAMA MUAMUZI WA MASUALA MUHIMU MAISHANI

Wanawake huchukua nafasi kubwa katika uamuzi wa masuala nyeti maishani. Japo nafasi hii haionekani bayana, lakini mengi yanayotekelezwa na wanaume huidhinishwa na wanawake, kisiri au dhahiri. Kauli kuwa 'Kando ya ufanisi wa kila mwanamume kuna mwanamke' inasadifu hapa. Hawaa katika *Utendi wa Adamu na Hawaa* aeleza kuwa kusudi kubwa la kutaka kula matunda ya mti wa kati ilikuwa kupata wana, kuendeleza jamii ili waongezeke, kwani hili lingewaletea furaha.

Ubeti wa 224:

Yapasa tujitahidi

Kusudi yetu tuzidi

Kwa wana tuwe suudi

Tutengeze jumuiya.

Kwa kula tunda la mti wa kati wangepata bahati ya kupata watoto na hivyo kuongezeka. Ubeti wa 225:

Wana wajae peponi

Kwamba tuwe furahani

Malaika muumini

Wingi sisi kuzidiya.

Suala la kupata watoto na hivyo kuongeza jamii lilitokana na Hawaa na si Adamu, Hawaa ndiye aliyeamua. Taswira mpya ya mwanamke tunayopata katika matini hii ni kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu , ana hekima, ni shujaa na kuwa maamuzi na mielekeo muhimu maishani humtegemea yeye. Hili linaafiki madhumuni ya mtafiti. Matini hii hali kadhalika iliandikwa ikifuata mafundisho ya kidini na hii ni dhihirisho tosha kuwa dini haimbamgui wala kumkandamiza mwanamke . Hili linaafikiana na nadharia tete ya mtafiti.

Katika *Paradise Lost*, tunaona kuwa baada ya Adamu na Hawaa kufanya dhambi ile ya kwanza, walikosana na kulaumiana. Wakiwa duniani walikofukuzwa na Mungu, tunaona Hawaa akichukua hatua muhimu ya kurudiana na Adamu. Kurudiana lilikuwa ni suala muhimu kwao na Hawaa ndiye aliliasisi. Hili laafiki nadharia tete ya mtafiti kuwa kuendelea au kufaulu kwa maamuzi ,mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea

mwanamke . Hatujui kungetokea nini kama mwanamke hangechukua hatua hii muhimu ya maridhiano.

Hakuna mume aliye shujaa kwa mkewe na wanaume wengi katika ndoa wanamilikiwa na kutawaliwa na bibi zao. Si ajabu utakuta wengi hutoroka nyumbani na kwenda vilabuni kwa kuogopa 'Thatcher' wao. Wanawake huamua na kudhibiti mengi katika ndoa.Hivyo ndoa ni faraja zaidi kwa wanawake kuliko kwa wanaume.

Maillu (1988) katika *Our Kind of Polygamy* asema:-

> Ulevi unaoendelea vilabuni kila jioni waweza kuwa dhihirisho la vita vya kisaikolojia mwanamume anavyopigwa na mkewe nyumbani.

Mwanamume hupiga, mwanamke huroga, urogi wake ni wa maneno na kauli kali.

Ni kweli kuwa aghalabu mwanamke hanazo nguvu za misuli kama mwanamume , lakini kauli zake huwa za ukali na huweza kumjuvya mwanamume yeyote. Hizi ni nguvu katika unyonge na hili linaafiki nadharia tete ya mtafiti na madhumuni ya utafiti.

Katika Biblia , ingawa Isaka alitaka kumbariki Esau, Rebeka aliamua ni nani atabarikiwa. Alimfanyia Yakobo njama kali iliyomfanya abarikiwe na Isaka. Isaka hakuweza kutegua kitendawili hiki cha 'mwanamke'. Hili linaafiki suala

la utafiti. Uamuzi huu ulifanya Yakobo baadaye kuwa mwanzilishi wa Taifa la Israeli (Mwanzo 27:1-33)

Biblia hapa , kwa kumpa Rebeka ushindi dhidi ya mumewe Isaka, inamwinua na kumtukuza mwanamke , haimgandamizi. Hili linatusaidia kumsawiri mwanamke upya – mwamuzi wa masuala muhimu maishani - kama ilivyokuwa lengo la utafiti.

Maendeleo na mafanikio mengi nyumbani hutengemea maamuzi ya mwanamke. Kwa yakini ndoa nyingi zingesambaratika kama si uamuzi wa mwanamke kuvumilia kukuru kakara za ndoa.Mtafiti aliweza kuwahoji wanaume wa makamo kuhusu swala la kifo katika ndoa, na wengi walitoa rai kuwa wangelipewa uchaguzi,wangelipendelea wafe kabla ya wakeze. Sababu kubwa walisema ni kuwa wanawake ndio bora katika ulezi wa watoto na jamii kwa jumla. Hata hivyo,wahojiwa wote waliafikiana kuwa rai hii haina mashiko uzeeni. Rai hii inatupa mwanga kuwa ndoa huendelezwa na wanawake na katu haimgandamizi. Taswira ya mwanamke hapa ni kuwa yeye ni jabali la kuegemea katika ndoa na hili linasadifu madhumuni ya utafiti.

Viongozi wengi wangekwanguliwa kutoka uongozini kwa makosa mbalimbali, lakini wake zao huamua kuwatetea na kusimama kidete nyuma yao na hii hufanya viongozi hawa waepuke matatizo, hata kama ni kwa muda. Mfano

mwafaka ni pale ambapo katika mwaka wa 2000, mmoja wa waziri katika serikali ya Moi alishtakiwa kwa kumnajisi msichana mdogo wa miaka 14, binti Florence Nangini Mpayei na kumpachika mimba. Banati huyu, akisaidiwa na wakili wanaowatetea wanawake (FIDA), alienda kortini akiwa na mwanaye aliyemlanda waziri huyo, Sunkuli, kama reali kwa ya pili.

Yawezekana Sunkuli na mkewe waligombana kisiri, lakini picha iliyojitokeza kwa umma ni ya mke anayempenda mumewe,na anayesadiki mumewe anaonewa. Ushahidi shadidi ulikuwepo kuonyesha Sunkuli alikuwa na makosa, lakini mkewe aliupa kisogo uhalisi huu ili adumishe ndoa yao. Huu ulikuwa ni uamuzi wa ajabu na ulisaidia kumwokoa Sunkuli na kudumisha ndoa yao.Ndiyo, uamuzi huu ulificha ufasiki, lakini hata hivyo ukweli ungekuwa na madhara makubwa kwao,na aila yao kwa jumla. Wake wanaokataa kuwa na uamuzi kama huu huishia kuvunja ndoa zao na, kwa kiasi kikubwa, kuwaletea watoto wao jinamizi.

Maoni ya mtafiti ni kuwa ni heri uwongo unaosalimisha na kuokoa maisha kuliko ukweli unaoua na kuangamiza. Huu hata hivyo ni unyonge wa mwanamke.

(Tazama Daily Nation 26/5/2000, 10/6/2000, 24/6/2000)

Si Sunkuli pekee, viongozi mashuhuri kama aliyekuwa Rais wa Amerika, Bill Clinton, alipatwa na kashfa ya kimapenzi na Monica Lewnsky. Mkewe Clinton

hakuvunja ndoa yao na alisimama kidete nyuma ya mumewe na hivyo kutetea maslahi yao. Uamuzi kama huu si wa kijinga kama wengi wanavyofikiri, bali unaonyesha nguvu za mwanamke katika kuamua masuala nyeti . Uamuzi wa kuvumilia madhila ya ndoa si unyonge, bali ni kipawa alichopewa mwanamke na Mungu na huhifadhi taifa, kwani taifa hujengwa juu ya misingi ya familia.

Mambo mengi wanaume wanayotenda au kusema hutokana na uamuzi na ushawishi wa mwanamke.Tajriba hizi pamoja na matini mtafiti alizodengua zinamsawiri mwanamke upya kama ilivyokuwa kusudio la utafiti kuwa: Kuendelea au kufaulu kwa masuala muhimu maishani humtengemea mwanamke. Mke wa Sunkuli na mke wa Clinton walikuwa na uamuzi wa kuwaangusha mafahali hawa wa kisiasa nyakati zile,lakini uamuzi wao uliwapa kinga na nyadhifa zao zikahifadhika, japo walengwa wenyewe walikuwa wamezichafua.

Kama Hawaa, mke wa Ayubu katika Biblia anamchochea mumewe mpaka anaanza kushuku uwezo na nguvu za Mungu. Matamshi yake yanamfanya Ayubu kuelewa zaidi juu ya Mungu - anafunguliwa macho. Mkewe alikuwa amemshawishi amwasi Mungu, kisha afe kwa sababu ya tanzia na maradhi yaliyokuwa yamemsibu. Ingawa Ayubu alimwita mkewe mpumbavu,

mwishowe alikuja karibu kufuata ushauri huu. Kwa kulaani siku aliyozaliwa, amlaani Mungu, kwani Mungu ndiye aliyempa uhai. Nadharia tete ya mtafiti kuwa mwanamke huathiri au kubatilisha maamuzi muhimu maishani ni sadikifu. Matini ya *Parauise Lost* imeandikwa chini ya misingi ya Biblia .

Khadija katika Koran ni mwanamke aliyechukua uamuzi ambao ulibadilisha maisha yake. Mwanamke huyu alikuwa mfanyi biashara na kwa miaka kadhaa, alikuwa amemwajiri Mtume Mohamed kama msimamizi wa biashara na mambo yake, hivyo alikuja kumjua vizuri. Khadija alikuwa na nafsi thabiti, alijitegemea kiuchumi na kijamii, hivyo alikuwa huru. Uhuru huu unadhihirika katika uamuzi wake wa kujichagulia mume. Alifanya uamuzi kuwa ataolewa na Mohamed, aliyekuwa mdogo wake kwa miaka 15. Khadija alituma mwanamke aliyeitwa Neffissa kama mshenga kwa Mohamed. Katika kitabu cha El Tabakat, El Kobr, mwandishi, Mohamed Ibn Saad anaripoti kuwa mjumbe Neffissa alisema:

> "Khadija alinituma kwa Mohamed
> kisiri akipendekeza amwoe,
> na alifanya hivyo" (Saadawi 1980).

Matukio ya kijamii na kisiasa yaliyokuwepo wakati ule , kama vile hali za kivita, yaliwafanya wanawake wengi kuwa wajane na kukosa waume.Uamuzi huu wa Khadija ulihitaji ujasiri, hekima na moyo thabiti .

Maandiko haya yanatusawiria mwanamke upya na kwa njia chanya,kama ilivyokuwa kusudi la utafiti : Kuwa mwanamke ni mwamuzi wa masuala muhimu maishani na kuwa anazo nguvu nyingi katika unyonge wake.

Dini, kama tulivyotaja, inampa mwanamke hadhi na fursa ya kuamua mwaswala muhimu maishani. Katika Biblia tunapata kisa cha Isaka na mkewe Rebeka. Ingawa Isaka alikusudia kumbariki Esau, Uamuzi huu haukufaulu, kwani Rebeka ndiye aliyeamua wa kubarikiwa. Kwa hekima, ushujaa na ukakamavu wa moyo thabiti, Rebeka alimwelekeza Yakobo atakayofanya ili abarikiwe, na hilo lilifanyika. Uamuzi huu wa Rebeka dhidi ya ule wa Isaka ulimuinua Yakobo ambaye hatimaye alikuja kuwa mwanzilishi wa taifa la Israeli, na babu wa masiha Yesu. Dini hapa imempa mwanamke hadhi kubwa , haikumkandamiza .Uamuzi wa Rebeka ndio ulioamua ukoo wa Yesu na hii ni dhihirisho kuwa masuala muhimu maishani na katika historia humtegemea na yalitegemea mwanamke.

Sipora katika Biblia kitabu cha Kutoka 4: 24-26 anamwokoa Musa kutokana na ghadhabu za Mungu. Mungu alikusudia kumuua Musa, lakini Sipora akakata govi ya zunga la mwanaye. Hili lilituliza ghadhabu za Mungu

... hakika wewe u bwana arusi wa damu kwangu ....

Hiki kilikuwa kitendo cha ujasiri. Mwanamke ana nguvu nyingi kiasi cha kumkabili Mungu na kufanikiwa ! Anabatilisha uamuzi wa Mungu ! Hili ladhihirisha kuwa mwanamke anaweza kutekeleza lolote maishani.

Kudengua maandishi haya ya kidini kunasadifu nadharia tete ya mtafiti na madhumuni ya utafiti kuwa kinyume na inavyochukuliwa,dini haimgandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi.Hali ya baadaye ya Musa iliamuliwa na mwanamke - Sipora. Kama Sipora hangeingilia kati ya Mungu na Musa , huo ungekuwa mwisho wa Musa na ukombozi wa wana wa Israeli .Ni wazi basi kuwa kuendelea au kufaulu kwa masuala muhimu maishani humtegemea mwanamke.

## 4.5 MWANAMKE KAMA MTOAJI WA MAJINA

Jina ni neno la kumtaja mtu au kitu. Majina yanayopewa watu huwa na maana na makusudio mbalimbali katika jamii mbalimbali ( King'ei 2005). Mbiti Katika *African Religious and Philosophy*(1975: 118-120) anasema kuwa, kwa kawaida, wanawake katika tamaduni za Kiafrika ndio waliowapa wana majina na hili lilitegemea mambo mengi kama vile uana, wakati wa kuzaliwa (usiku, mchana, asubuhi au jioni),hali ya anga (kiangazi, mvua, kipupwe, mapukutiko), mahali pa kuzaliwa ( njiani, nje,msituni, shambani), ukoo, majira, hali ya mazingira na kadhalika.

Utoaji wa majina ulianza na Adamu baada ya yeye kuumbwa.

Mwanzo 2:19-20

... Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika Ardhi

kila mnyama wa msituni na kila ndege wa angani,

akamletea Adamu ili aone atawaitaje,

kila kiumbe hai,jina alilokiita Adamu

likawa ndilo jina lake....

Adamu,hali kadhalika, ndiye aliyempa mwanamke jina, Hawaa - kumaanisha mama wa viumbe wote.

Katika *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa*, faslu ya tatu beti za 106 mpaka 127 zinatuonyesha Adamu akitoa majina kwa vyote vilivyoumbwa na Mungu wakiwemo malaika.

Ubeti wa 113-114

Huambiwa ataje nyama

Wa anga na chini hima

Na anaowafahamu

Wa bara hadi wa pwaa.

Ubeti wa 114

Adamu akawataja

Pasipo kungojangoja

Moja baada ya moja

Bila ya kuwakoseya.

Adamu hapa anatoa majina siyo tu kwa wanyama na ndege, bali pia kwa nafaka, miti na nyota kama ubeti wa 115-117 unavyoeleza.

Katika beti za 118-121, mtunzi anatueleza kuwa Adamu aliwataja malaika wote kwa majina yao na kazi zao kwa Mungu. Hili ni dhihirisho kuwa Mungu alikuwa amempa elimu azizi.

Ubeti wa 118:

Akatakiwa kunena
Ya malaika majina
Wote anaowaona
Hapo wamehudhuriya.

Ubeti wa 121:

Kawataja majinao
Kadhalika sifa zao
Na kazi kwa Mola wao
Na ibada zao piya.

Ingawa Adamu, alitoa majina awali, nafasi yake baadaye inachukuliwa na Hawaa katika kutoa majina ya watoto. Hawaa ndiye aliyetoa majina ya watoto waliozaa na hii ni dhana ghadi ya wanawake wote duniani. Hii inadhihirisha nguvu na uwezo alionao mwanamke.

Iliana Pardes (1993:41) *Countertraditions in the Bible* asema kuwa ingawa Hawaa alipewa jina na mwanamume, yeye sasa ndiye anayetoa majina kwa watoto.

<u>Mwanzo 4:1-2</u>

Adamu akamjua Hawaa mkewe, naye

Akapata mimba, akamzaa Kaini,akasema.

Nimempata mtoto mwanamume kwa bwana.

Akaongeza akamzaa ndugu yake,Habili.

Huku kusema "Nimempata mtoto kwa bwana" kunatupa mwanzo wa utoaji wa majina kwa akina mama. Kupata hapa ni sawa na kuumba.

Utoaji wa majina, haswa unapoandamana na uneni, huashiria mengi kuhusu anayetoa kuliko anayepewa jina; kwa kuweza kujieleza kupitia utoaji wa majina, mwanamke anakuwa kiumbe bora kuliko mwanamume. Huu ni utamalaki mkubwa wa mwanamke katika ndoa na juu ya mumewe. Tunarejelea Biblia hapa kwani ndio msingi wa matini ya *P.L*

Pardes (1993) anaendelea kueleza kuwa baada ya Hawaa kumzaa mtoto wao wa tatu Sethi, Hawaa alikubali nguvu / uwezo wa Mungu, lakini hili halikumaanisha alikubali atawaliwe na Adamu. Bado mama huyu alisawiri kizazi kama tendo lililokuwa baina yake na Mungu. Ukubalifu huu hujitokeza katika kuwapa wana majina na maneno yanayoandamana, na ni usadifu

kuwa mwanamke anazo nguvu nyingi na huamua mkondo wa masuala muhimu maishani.

Mwanzo 29:32-39 :

> Lea akapata mimba akazaa mwana, akampa jina lake, Reubeni, maana alisema, kwa kuwa Bwana ameona teso langu, sasa mume wangu atanipenda. Akapata mimba tena akazaa mwana akasema, kwa Bwana amesikia ya kwamba mimi sikupendwa, amenipa na huyu. Akamwita Simeoni. Akapata mimba tena, akazaa mwana, akasema, Basi wakati huu mume wangu ataungana nami kwa sababu nimemzalia wana watatu. Kwa hiyo akamwita jina lake Lawi. Akapata mimba tena akazaa mwana. Akasema. Mara hii nitamsifu Bwana; kwa hiyo akamwita jina lake Yuda; akaacha kuzaa.
>
> Mwanzo 30:24
>
> Mungu akamkumbuka Raheli, Mungu akamsikia, akamfungua tumbo. Akapata mimba, akazaa mwana, akasema Mungu ameondoa aibu yangu. Akamwita jina lake Yusuf, akisema, Bwana aniongeze mwana mwingine.

Katika kitabu cha Samueli wa kwanza, kifungu cha kwanza, mstari wa ishirini : kisa cha Hana, mkewe Elkana kuhusu utoaji wa jina kinaeleza:



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Ikawa wakati ulipowadia, Hana akachukua mimba,

na kuzaa mtoto mwanamume akamwita jina lake Samweli,

akasema kwa kuwa nimemwomba kwa Bwana.

Modondoo haya yote yanadhihirisha kuwa kitendo cha kuwapa majina watoto kinampa mwanamke fursa kubwa zaidi kuliko mwanamume katika ndoa na hivyo ndoa haimgandamizi mwanamke.

Binti Farao katika Biblia kitabu cha Kutoka anaonyesha nguvu za kike pia katika utoaji wa jina kwa mtoto aliyemwokota mtoni na kumlea kama wake.

Kutoka 2:10

... Akamwita jina lake Musa, Akasema; Ni

kwa sababu nalimtoa majini.

Hatuoni mwanamume akihusika katika utoaji wa majina .Hii ni dhihirisho la uwezo mkubwa alionao mwanamke na ambao amepewa na dini.

Utoaji wa majina katika utu uzima huweza kuonyesha mabadiliko ya hulka au nafsi. Mtoto wa Isaka katika Biblia, aliyeitwa Yakobo, alikuja kubadilishwa jina na kuitwa Israeli na Mungu. Jina hili liliashiria mabadiliko ya kitabia, kama 'kuzaliwa' upya, kwa maana anaonekana kuingia katika kitengo cha juu zaidi baada ya kujulishwa kuwa atakuwa baba wa Taifa.Katika jamii nyingi za Kiafrika, mwanamke anazo nguvu za kutoa majina kwa uzao wake.

## 4.6 MWANAMKE KAMA SHUJAA

Ingawa tumeshajadili mwanamke kama mwenye nguvu, hebu sasa tumtazame kwa ushujaa. Si lazima shujaa awe mwenye nguvu, wala mwenye nguvu awe shujaa. Kulingana na kamusi ya Kiswahili Sanifu, shujaa ni:-

> Mtu mwenye moyo thabiti anayeweza
> kukabili mambo, hata kama ni ya hatari.
> Jasiri, nguli, jogoo, jabali, ghazi,nyamaume.

Katika tendi zote mbili tulizotalii, yaani *Paradise Lost* na *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa,* waandishi wote wawili, japo walitengana kitalifa kama mbingu na ardhi, japo walikuwa wa dini tofauti, japo waliishi nyakati tofauti, lakini wote wanamsawiri Hawaa kama mwenye ushujaa mwingi. Kitendo cha Hawaa katika *Utenzi wa Adamu na Hawaa* cha kumwacha Adamu kwa muda mrefu na kutembea peponi peke yake ni ujasiri mkubwa. 'Kupotea' kwa Hawaa kunampa Adamu usumbufu, kama vile ambavyo kila mwanamume huhisi anapopotelewa na mpenzi au mke wake (Ubeti wa 155-156). Maswali Adamu anayomuuliza Hawaa ni yale yale ambayo kila mwanamume humuuliza mkewe anaporudi amechelewa - "Sasa ni saa ngapi? Unatoka wapi?" (Ubeti wa 157) na nikiongezea - "Ulikuwa na nani? Mbona hukunijulisha wakati ukienda?" na kadhalika.Hawaa kwa ushujaa wa mtu aliyetenda alilotenda kwa uamzi wake anamjibu Adamu:-

Ubeti wa 158

Nili ni matembezini

Kitazama nyingi shani

Zilizo humu peponi

Ndipo nikakawiliya.

Majibu haya ya Hawaa ni ruwaza ya majibu ambayo wanawake wote hutoa wakiamua kutenda jambo. Huwa wana sababu na majibu ya kutoa pindi waulizwapo na waume wao au wapenzi wao.

Hawaa anapotunda tunda la mti ulioharamishwa, anaonyesha ushujaa.

Ubeti 316.

Bibie akainama

Hilo tunda kulichuma

Mtu akilitazama

Ute humdondokeya.

Hawaa kutaka kujua kwa nini Mungu akaharamisha kula matunda ya mti wa kati kunaonyesha ujasiri na moyo thabiti na huu ni usawiri upya wa mwanamke kama shujaa (Ubeti wa 212-214).

Katika utendi wa *Paradise Lost*, kitabu cha tisa, tunaona Hawaa akitaka kujua kitakachotokea pindi walapo matunda ya mti wa kati. Huu ni ushujaa mwingi, ni kama anamkabili Mungu kwani amri ya kutokula matunda yale ilitokana na

Mungu.Tendo la kumkabili Mungu laashiria ushujaa na ujasiri mkubwa.Sipora, kama Hawaa,alionyesha hili kwa kumkabili Mungu.

Saadawi (1950:125) asema mwanamke aliyeitwa Nessiba Bint Kaab alipigana kwa upanga wakiegemeana na Mtume Mohamed katika vita vya Ahad. Mwanamke huyu hakugura vita hadi alipojeruhiwa mara kumi na tatu ... Mohamed alimtukuza na kusema, "Nafasi inayochukuliwa na mwanamke huyu *ni ya juu kuliko ile ya wanaume." Koran, kama Biblia, inatusawiria* mwanamke kama shujaa. Dini haimkandamizi mwanamke, imemwinua. Saadawi anaendelea kutujulisha kuwa Om Salayem Binti Mathan alifunga hanjari (sime) kiunoni, juu ya mimba na pia alipigana katika kiwango cha Mohamed na wafuasi wake. Huu ni ushujaa na ujasiri mwingi-kupigana akiwa mja mzito ! Mtafiti amerejelea maandiko matakatifu kwani ndio msingi wa tendi ailizochanganua.

Mke wa mwisho wa Mohamed, Aisha, kama tulivyokwisha taja, alipigana katika vita vingi na alikuwa mwana harakati wa kisiasa, na harakati zingine za kijamii na kielimu.

Mifano hii yote kutoka dini ya Kiislamu yamsawiri mwanamke kama 'jogoo'.Allah kupitia Mtume Mohamed asema, "Sijaona viumbe wachache wa akili na dini walio na uwezo wa kuwashinda wanaume wenye busara na mantiki kuliko wewe (mwanamke) (Saadawi 1980).

Katika Biblia kitabu cha Mwanzo, tunaona kisa cha ajabu ambapo baada ya Lutu kusalimika toka Sodoma na Gomora akiwa na binti zake wawili, hawa walifanya mzengwe ili waendeleze kizazi cha baba yao. Kwa ujasiri mwingi, walimlewesha baba yao, naye akajamiiana nao bila kujua. Binti mkubwa alipata mimba akazaa mwana Moabu. Huyu ndiye baba wa Wamoabu hata leo. Mdogo pia alipata mimba kwa kujamiiana pia na babake na akapata mimba akamzaa Benami, naye ndiye baba wa Waamoni hata leo (Mwanzo 19: 30 - 38).

Kisa kingine cha ujasiri na ushirikiano wa wanawake kinapatikana katika Biblia,hadithi ya Lea na Raheli, banati wa Labani. Yakobo alimfanyia Labani kazi miaka saba ili amuoe Raheli, miaka aliyoiona kama siku saba, kwa sababu ya mapenzi yake kwa Raheli. Usiku wa nikahi, Labani alimtwaa binti yake mkubwa, Lea, badala ya Raheli kuwa mke wa Yakobo .Yakobo hakutambua kuwa aliyekuwa naye kitandani si Raheli. Kivipi? Bila shaka dada Lea alikuwa amefunzwa mengi na Raheli jinsi ya kufanya ili Yakobo amwone Lea kama Raheli. Raheli alikuwa chini ya kitanda akimsaidia Lea kwa mengi usiku huo wa nikahi. Ushirika kama huu ni ujasiri mkubwa kutoka kwa dada hawa wawili.

Yakobo alilazimika kumfanyia Labani kazi miaka mingine saba ili amuoe Raheli. Dada hawa wawili hivyo waliishia wote kuolewa na Yakobo.

Yakobo aliendelea kufanya kazi kwa Labani lakini alidhulumiwa sana (Mwanzo 31:5-7).

> Naona uso wa baba yenu , kwamba
>
> hanitazami vema kama jana na juzi....
>
> Nanyi mmejua ya kwamba kwa nguvu
>
> zangu zote nimemtumikia baba yenu.
>
> Na baba yenu amenidanganya , akabadili
>
> mshahara wangu mara kumi....

Lea na Raheli walishirikiana wakati walipoona baba yao, Labani anamdhulumu mume wao na wakaamua kutoka nyumbani mle mwa Labani,baba yao.

*Mtafiti ametoa mifano hii ya kipekee kuonyesha* ujasiri na ushirikiano mkubwa kati ya wanawake. Banati hawa wa Lutu walionyesha uthabiti wa moyo. Je, ingekuwa ni ghulamu wawili, wangefanya mpango kama huu na kuzini na mama yao?

Katika maisha, ni wazi kuwa mama na binti huweza kuzungumzia siri zao za kindani kabisa kinyume na baba na ghulamu ambao hawafunguliani roho zao. Hali hii ya wanawake kuweza kushirikiana katika siri zao inadhihirisha ujasiri wa hali ya juu, na ni sifa kuu ya wanawake. Hii pia yaweza kueleza kwa nini katika jamii zetu za Kiafrika mitara iliweza kuendelea. Wanawake

walivumiliana, kuliwazana, na waliweza kuishi pamoja kinyume na wanaume.(Hali hii hata hivyo imepitwa na wakati siku hizi).

Katika Biblia kitabu cha Kutoka: 1: 2, tunapata kisa cha wakunga wawili ambao wanaonyesha ujasiri kwa kukataa kutimiza amri ya Farao, kwa kutoa hekaya na ngano za ukunga kama vijisababu.

> Kisha mfalme wa Misri akasema na wazalishaji wa Waebrania; mmoja jina lake aliitwa Pua; akasema wakati mwazalishapo wanawake wa Kiebrania na kuwaona wa katika kuzaa, ikiwa ni mtoto mwanamume, muueni, bali akiwa ni mtoto mwanamke; na aishi … Wasifanye kama walivyoamriwa na huyo mfalme wa Misri … basi mfalme wa Misri akawaita wazalishaji na kuwauliza kwa nini, kufanya jambo kama hili… wazalishaji wakamwambia Farao; ni kwa sababu hao wanawake wa Kiebrania si kama wanawake wa Misri, kwa kuwa ni hodari hao huzaa kabla mzalishaji hajapata kuwafikia (Kutoka 1: 15 -19).

Wakunga hawa wanamwambia Farao kile anachotaka kusikia na kwa njia hii wanaokoa si tu malaika wa Kiebrania, bali pia nafsi zao ---- Wanawake wa Kiebrania si kama wa Kimisiri, wao ni kama wanyama na waweza kujifungua bila utarazaki wa ukunga.

Katika Kutoka:1: 2, tunaona Farao sasa akiwaambia watu wake wawatupe watoto wote wa kiume wa Kiebrania mtoni. Mamaye Musa anaonyesha ujasiri kwa kujifanya kutii amri ya Farao : - Musa alitupwa mtoni alikookotwa na Binti Farao.

Binti Farao pia anaonyesha ujasiri pale anapomwokoa na kumlea mtoto wa kigeni nyumbani mwao. Utoaji jina kwa mtoto huyu kwaonyesha pia ushujaa na ukakamavu wa binti huyu.

.... akamwita jina lake Musa, akasema;

Ni kwa sababu nalimtoa majini (Kutoka 2: 10).

Mifano aliyotoa mtafiti inamsawiri mwanamke upya na kwa tariki chanya. Biblia, kitabu kitakatifu, kinampa mwanamke nyadhifa kubwa kuliko mwanaume katika ndoa . Kutoa jina kwa mtu au kitu ni tariki moja ya kumtamalakii au kukitamalaki .Mbwa,ng'ombe, farasi na viumbe wengine wasio na akili kama binadamu huweza kuonyesha hisia pindi waitwapo kwa majina yao,seuze binadamu ? Kwa kutoa majina kwa watoto, wanawake

huwa na umiliki mkubwa juu yao.Wao huwa na sababu za kutoa jina fulani, na mwanaume hana jingine ila asalimu uamuzi huu.

## 4.7 MWANAMKE KAMA MPATANISHI

Mwanamke ni daraja katika mahusiano yoyote yale. Mwanamke mweledi huweza kumuunganisha mumewe na Mungu, jamii zake na hata wote wanaomjua mumewe.

Ikiwa mwanamke anamtaka mwanamume, anaweza kumjenga lakini akimchukia, anaweza kumbomoa kabisa.

Mke wa kwanza wa John Milton alipotaka, aliweza kumwacha mumewe japo Milton alimshawishi sana asiondoke. Powell hata hivyo alipotaka, aliweza kumshawishi Milton na hivyo wakarudiana. Hapa akawa mpatanishi tena katika ndoa yao.Matini hii basi inatusaidia kumsawiri mwanamke upya kama mpatanishi.

Katika maisha ya ndoa, mama ndiye mpatanishi kati ya baba na watoto. Kwa kawaida mama hukaa na watoto kwa muda mrefu na mwanamke mzuri hulea watoto wamheshimu baba hata kama ni mlemavu. Hata baba awe kidudu cha aina gani, katu hatabadilika, bali atabakia tu baba. Katika hali hii, mwanamke anakuwa mpatanishi kati ya baba na watoto. Katika familia ambapo mama anamchimba baba kwa watoto, hata baba yule awe na

uzuri wa malaika, watoto watamdharau na kumwona kama kinyaa. Kule kumbeba mwana kwa miezi tisa, kumnyonyesha na kumlea humpa mama uwezo mkubwa juu ya mtoto kuliko baba. Kiunga mwana kati ya mama na mtoto hudumu milele.

Tukiendelea kuangazia maisha ya jamii, tunaona kuwa mama huwa msiri mkubwa wa watoto kuliko baba. Wanapoendelea kukua, huweza kutatua na kuwahimiza watoto katika kujitambua utu uzima unapogonga mlango. Hivyo mama huwa ni kiungo muhimu cha upatanishi wa maisha ya ujana na utu uzima kwa watoto. Baba hujulisha tu mambo yakiwa yameiva au yakizidi unga.

Katika Biblia Wafalme wa Kwanza :18- 20, Ahinoam alimtukana Daudi, mfalme wa Israeli, naye Daudi akataka kumwangamiza, lakini mkewe Abigaili aliingilia kati na kumuomba msamaha kwani mumewe alitenda vile kwa upumbavu. Hapa mwanamke akawa mpatanishi.

Mke wa tatu wa Milton, Elizabeth Minshull anasawiriwa kama mpatanishi na mwenye hekima. Alielewa matakwa ya Milton na ya binti zake Milton. Kwa hekima nyingi aliweza kumtafutia Milton msaidizi wa kazi nao binti wake akawapatia kazi ya udarizi. Kwa njia hii, aliweza kuwapatanisha baba na binti zake wakaishi vizuri. Alisaidia pande zote mbili.

## 4.8 KIISHILIO

Imebainika kutokana na hoja mtafiti alizojadili kuwa mwanamke ni kiungo muhimu katika maisha na kamwe hawezi kupuuzwa. Usawiri huu mpya wa mwanamke umetokana na mzinduko mkubwa kuhusu nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya kijamii. Sifa zilizotajwa zinampa mwanamke nguvu na uwezo wa kuamua mielekeo na mikondo muhimu katika maisha, kama ilivyokuwa katika nadharia tete ya mtafiti ambayo sasa ni sadikifu. Mwanamke amesawiriwa kama mwenye hekima, nguvu, mwamuzi wa masuala muhimu maishani, mtoaji wa majina, shujaa na mpatanishi. Hizi ni sifa chache tu miongoni mwa nyingi alizonazo mwanamke.

Imebainika wazi kuwa taswira za mwanamke zinazojitokeza katika *Paradise Lost* na *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* zinamwonyesha mwanamke kama kiumbe mwenye nguvu na wala si dhaifu. Hawaa, kwa kumfanya Adamu amtii yeye na kula tunda lililoharamishwa, anaonyesha ushindi mkubwa dhidi ya Mungu kwani amri ya kutokula tunda ilitokana na Mungu.Hoja ya kutaka kujua kitakachotokea baada ya kula tunda kunaonyesha ujasiri na kiu ya kupata hekima.Hili linaafiki madhumuni ya utafiti.

Tendi hizi mbili alizorejelea mtafiti katika utafiti huu zimeandikwa kwa kuegemea vitabu vitakatifu-Biblia na Koran, na kwa kudengua baadhi ya

maswala ya kike yaliyomo mle,mtafiti ameweza kumsawiri mwanamke upya na kwa njia chanya. Mwangwi wa matendo ya Hawaa umeathiri mielekeo ya wanawake kama mtafiti alivyojadili.Hawaa ni kiakisi au dhana ghadi ya wanawake wote wa baadaye.Kama Adamu,wanaume wengi hufanya mengi kuwaridhisha wake au wapenzi wao.

Ili kufaulisha kazi yake,mtafiti alitumia nadharia changamano ya Unisai wa Kidenguzi.

Masuala mengi mtafiti aliyorejelea katika matini mbalimbali, na ambayo yalihusu wanawake, yaliweza kuelezeka bila kurejelea muktadha.Masuala mengi yalikuwa ya uwazaji na hayakujifunga kwenye kaida za uhalisia.

Mihimili changamano ya nadharia ya Unisai wa Kidenguzi imemwezesha mtafiti kutimiza madhumuni ya utafiti. Mtafiti amebainisha kuwa tungo za *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* na *P.L* zinamsawiri mwanamke kama kiumbe mwenye nguvu.Dini na ndoa ni asasi zinazofikiriwa kuwa zinamkandamiza mwanamke, lakini hili si kweli kama vile mtafiti alivyobainisha. Mihimili hii hali kadhalika imemwezesha mtafiti kumsawiri mwanamke upya na kwa njia chanya – ni mwenye nguvu,ana hekima kushinda mwanaume, ni mwamuzi wa masuala muhimu maishani, ni shujaa, mpatanishi, na mtoaji wa majina .Fauka ya yote,ni mwepesi wa kutubu na mama wa viumbe wote.

Tungo hizi mbili ziliandikwa kwa kuegemea vitabu vitakatifu-Biblia na Koran,na urejeleaji kwa matini hizi takatifu ulisaidia katika kumsawiri mwanamke upya.

# SURA YA TANO

## 5.0 Utangulizi

## 5.1 Mahitimisho

Mtafiti amethibitisha malengo ya utafiti kwamba mwanamke anazo nguvu nyingi katika unyonge wake, na kuwa anachangia mengi katika kufanikisha mikondo muhimu maishani. Bila ya mwanamke ni bayana kuwa aila nyingi zingesambaratika na kwa kiwango fulani taifa.

Mtafiti ameaua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika dini mbili tofauti katika nyakati tofauti na mazingira tofauti. Kwa yakini mtafiti amethibitisha kuwa dini kinyume na inavyosingiziwa haimgandamizi mwanamke bali imempa nguvu nyingi.Nguvu hizi kwa wengi huonekana kama udhaifu.

Ni wazi kuwa nafasi ya mwanamke kama shujaa , mtoaji wa majina, mwenye hekima, mpatanishi, na mwamuzi wa masuala muhimu maishani imechunguzwa jinsi ilivyosawiriwa katika matini nyingi. Mtafiti amethibitisha kuwa dini za Uislamu na Ukristo zina uwiano mkubwa na zote zina mtazamo karibu sawa kumhusu mwanamke.

Ni matarajio ya mtafiti kuwa usawiri huu mpya wa mwanamke utakuwa na kuzidisha changamoto sio tu kwa waandishi wa fasihi, bali kwa jamii nzima ya

ulimwengu. Mwanamke akieleweka upya, na apewe nafasi anayostahili, maendeleo makubwa yataweza kupatikana.

Mtafiti anaonelea kuwa tariki faafu ya kubadilisha mitazamo hasi kuwahusu wanawake ni kuasisi elimu ya uana katika shule zetu, kuanzia zile za chekechea.

## 5.2 Hitimisho na matokeo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Unisai wa Kidenguzi ambayo ni nadharia changamano. Mtafiti alichunguza masuala yanayomhusu mwanamke kwa kurejelea *Paradise Lost* na *Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa.* Alizidengua matini hizi na kwa njia hii akaweza kumsawiri mwanamke upya.Usawiri huu ni kwa njia chanya .

Mtafiti aidha aliweza kurejelea matini na makabrasha anuwai zilizoeleza masuala ya Ufeministi. Haya kwa pamoja yalimwezesha kumsawiri mwanamke upya, kwani matini ni chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana bila kurejelea muktadha .

Mtafiti alikuwa na nadharia tete zifuatazo:

(i) Mwanamke anazo nguvu nyingi katika udhaifu wake : Mtafiti amedhihirisha hili kwa kutoa mifano ya Hawaa, Sara mke wa Ibrahimu, Rabeka, Delila na mifano mingine anuwai.

(ii)Kinyume na inavyochukuliwa na wengi, dini haimkandamizi mwanamke bali inamwinua na kumpa hadhi : Kitendo cha Hawaa cha kumfanya Adamu amtii yeye Hawaa, kuliko kumtii Mungu, kitendo cha Sipora cha kugeuza ghadhabu ya Mungu, vyote vinadhihirisho hadhi ya dini kwa mwanamke. Naumi na wajane wale wawili wanachukua nafasi kubwa katika ukombozi wa walimwengu, Khadija na Aisha wana jukumu kubwa katika maisha ya Mtume Mohamed.

(iii) Kuendelea ama kufaulu kwa maamuzi, mielekeo na mikondo muhimu maishani humtegemea mwanamke : Ingawa wanawake hawana nguvu za misuli, utafiti amethibitisha kuwa hii si hoja maishani. Wanawake wameweza kusababisha kuanguka kwa falme na hata mataifa, na hawana nguvu za kimwili. Maendeleo mengi ulimwenguni yamefanyika kwa sababu ya wanawake.Kwa yakini, wanawake ndio kichapuzi katika maendeleo yote ulimwenguni.

Utafiti umekwisha thibitisha nguvu za mwanamke ambazo wakati mwingi huonekana kama 'unyonge' : Hawaa anamkabili Mungu anapomshawishi Adamu ale tunda alilowakataza. Sara anamtamalaki Ibrahimu anapompa mashauri ya kuoa na baadaye ya kumfukuza Hajiri, mjakazi wao. Binti wa Lutu wanaonyesha ujasiri na hekima wanapoendeleza kizazi na baba yao.Delila alifaulu kumwangusha Samsoni pale ambapo wengi walishindwa. Sipora anamkabili Mungu na kumfanya abatili uamuzi wa kumuua Musa. Rebeka

anaamua kati ya Esau na Yakobo atakayebarikiwa. Khadija anafanikiwa kuolewa na Mtume Mohamed. Mke wa Ayubu anafanikiwa kumshawishi Ayubu kumwasi Mungu,( Ayubu kwa kulaani siku aliyozaliwa ni kama ana mlaani Mungu ,kwani ndiye hutoa uhai). Mifano hii yote inadhiirisha kuwa mwanamke ana nguvu nyingi. Nguvu zake hutokana na ufasaha wa kalima, hisi zinazoibuliwa na machozi, na viambata vya hisi za mwili.

Utafiti umedhihirisha pia kuwa ushirikiano wa wanawake hugeuza matukio ya kihistoria : Masiha Yesu alitokana na ukoo wa Daudi. Daudi ailizaliwa kutokana na ushirikiana wa wanawake wawili,Ruthu na Orpa. Lea na Raheli walishirikiana usiku wa nikahi ya Raheli na hivyo Yakobo kutoweza kutambua aliyekuwa naye usiku huo. Mifano hii na mingine inadhihirisha kuwa mikondo na mielekeo muhimu maishani humtegemea mwanamke. Ushirikiano wa wanawake huleta mageuzi maishani. Mifano mtafiti aliyotoa ya usawiri upya wa mwanamke imejikita katika vitabu vitakatifu. Hivi ndivyo vilivyokuwa msingi katika kuandikwa kwa tendi mtafiti alizochanganua. Usawiri huu upya umemwonyesha mwanamke akiwa na hekima, mpatanishi, mtoaji wa majina, Shujaa, na mwamuzi wa masuala muhimu maishani. Dini imempa mwanamke hadhi na sifa kubwa na hivyo haimkandamizi.

Taswira za mwanamke ziinazojitokeza katika tendi ambazo mtafiti ameziteua zimeonyesha bayana kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu.Vitendo

vya Hawaa, miondoko na kalima zake ni kiakisi na mwangwi wa wanawake wote duniani.

Mtafiti ameweza kutimiza malengo yake ya utafiti kwa kubainisha kuwa taswira zilizoko katika tungo za *Paradise Lost* na *Utendi wa M aisha ya Adamu na Hawaa* zinansawiri mwanamke kama mwenye nguvu. Aidha ameweza kuonyesha jinsi taswira hizi zinavyoathiri mielekeo ya wanawake.Kwa tariki hizi , ameweza kumsawiri mwanamke upya.

Nadharia tete alizoteua ni sadikifu na malengo ya utafiti yametoshelezwa.

## 5.3 MAPENDEKEZO

Mtafiti amechunguza usawiri upya wa mwanamke katika utendi wa *Paradise Lost na Utendi wa Maisha ya Adamu na Hawaa*, lakini bado kuna utafiti zaidi unaoweza kufanywa, haswa katika utendi wa *Paradise lost.*

Matumizi ya lugha ni mojawapo ya mada ambayo ina mengi ya kutafitiwa, hasa ikizingatiwa kuwa aliandika kwa Kingereza cha zamani.

Utafiti hali kadhalika unaweza kufanywa juu ya mwandishi wa *Paradise Lost*,yaani John Milton, uhusiano wake na maasi ya Uingereza, na fursa aliyochukua kama mshauri na karani wa serikali.

Utafiti pia unaweza kufanywa juu ya jinsi matukio ya kisiasa Uingereza yalivyomwathiri Milton katika maisha yake na uandishi wake.

## MAREJELEO


Andersan E. na Wolfe A. (1974 . *Women of the Bible*. Kesho Publication. Kijabe,Kenya.

Anderson, M.L (1997). *Thinking about women*.U.S.A.

Beauvoir, S (1972) *The Second Sex*. Harmondswonti. Penjuin Books.

Belsey C. na Moore J. (1997). *The Feminist reader*. Macmillan Press Ltd London, Great Britain.

Bouchier,D (1983).*The Feminist Challenge.The Movememt for Women's Liberation in Britain and the U. S.A*.London,Macmillan Press.

Bradfold, R (1992). *Paradise Lost*. Bristol ,U.S.A.

Chacha N.C (1980). ' Ushairi wa Abdilatif Abdala.' Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa ).

Danielson D. (Mh) (1989). *The Cambridge companion to Milton Cambridge* University Press, U.S.A.

David Loewenstein (1993); *Milton: Paradise Lost*. Cambridge University Press. London.

Farouk M.T (1971). *Uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili*. Oxford University Press.

Friendan. B. (1963). *The femine Mystiaque*. New York, Dell .

Gitau E.N (2005). 'Unyanyasaji dhidi ya mwamke katika Fasihi Andishi ya

Kiswahili.'Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Grelot P(1964) *Man and wife in Scripture* (Translated by Roseleen Brennau Compass Books- London.)

Harrow, W.K (1991). *Faces of Islam in Africa literature.*Hughes Merritty (mh).

Iliana Pardes (1993). *Counter traditions in the Bible. A feminist Approach.* First Havard University Press, U.S.A.

Kate, M (1977) *Sexual Politics*, Verso, London.

Katwiwa Mule (1991) 'Suala la mwanamke katika Tamthilia ya Kiswahili. Waandishi wa kike katika njia panda.' Tasnifui ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Keohame N. na wengine (1982). *Feminist Theory. A critique of Ideology.* Sussex:TheHarvestor Press Ltd.

Kimani W.C (2003) 'Suala la dhuluma dhidi ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili'.Tasnifu ya uzamili,Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kimani. N. na Rocha C. (1999). *Ufundishaji wa fasihi, Nadharia na Mbinu.*Jom Kenyatta. Foundation. Nairobi, Kenya.

Kimani Njogu (2007) (mh). *Kiswahili na Elimu nchini Kenya.* Kolbe Press, Nairo Kenya.

King'ei. K. na C.N.M Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Kenya Literature Bureau,Nairobi, Kenya.

Kithaka wa Mberia (1997). *Natala* . Marimba Publications Ltd. Nairobi, Kenya.

Lois Potter (1986). *A Preface to Milton.* Longman, Nairobi, Kenya.

Lovenduski J. et.al (1993). *Contemporary Feminist Politics*. New York, Oxford University Press.

Lugano,R.S(1989) 'Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi'.Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi,(Haijachapishwa).

Mailu D.G. (1988). *Our kind of Polygamy.* Heineman Kenya Ltd.

Mary Wollstonecraft (1792) – *A vindication of the Rights of Women*.

Mary Evans (mh) (1994*) The Woman question* , London.

Mathenge Joseph (2005) *Mwongozo wa Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Top Achievers Publication. Nairobi Kenya.

Mavise Rose (2007) 'Usawiri wa wahusika wa kike katika kazi za Zainabu Burhan.' Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mbatia Mwenda (2002) *Kamusi ya Fasihi* Nairobi, Standard Textbooks

-------------------------*2003)Mwongozo wa Walenisi*.Longorn Publishers, Nairobi

Mbiti .J. (1975 ) *African Religions and Philosophy* E.A P.H ,Nairobi, Kenya.

Mbughuni, P (1978).' From Oral to written._The Politicization of Kiswahili Literature.' Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Indiana. (Haijachapishwa).

Mekacha, R (1993 ')Mwanamke ni Ibilisi' katika Mulokozi et.al (wahariri) *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*,Dar-es-Salaam University Press.

Millet, J (1975) *Psychoanalysis and Feminism.*Harmondsworth, Penguin.

Mohammed S.A. (2001). *Mwongozo wa Kilio cha Haki*. Longhorn Publishers, Nairobi Kenya.

Moi. T (1985).*Sextual / Textual Politics . Feminist Literaly Theory* London Routledge.

Momanyi C. (1998) 'Usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili' Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

---------------- (2004) 'Ngome ya Nafsi' ,katika Wamitila,K.W (mh) *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyingine*.Nairobi Focus Publishers Ltd.

-------------- (2006). *Tumaini*. Vide muwa Publishers Nairobi, Kenya.

Muindi K. (1990) 'Usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya Said Ahamed Mohamed'. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mwachofi,A.K (1987) *Mama Ee*. Heinemann , Nairobi.

Ndungo C. M (1985) 'Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria katika fasihi ya Kiswahil.' Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa.)

---------------- (1997) 'Images of Women in African OralLiterature.A case of Gikuyu and Swahili Proverb.' Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Nyanchama . MB (2004). 'Matumizi ya Taswira na Ishara katika Sauti ya Dhiki (Abdalla A.) Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

P'. Bitek. Okot (1978). *Wimbo wa Lawino*. E.A.P.H . Nairobi.

Pierre Grelot (1964). *Man and Wife in scripture*. (Translated by Roseleen Brennau). Compass Books, London.

Saadawi N.E (1980). *The Hidden face o f Eve*. London, Zed Press.

Shaaban Robert (1951). *Kusadikika* . Evans Brothers. Nairobi, Kenya.

Tomaseveski .K. (1995 ). *Women and Human Rights*. Zed Books Ltd. London and New Jersey.

Tong. R.(1989). *Feminist Thought. A Comprehensive introduction*. Nairobi View Press.

Virginia Woolf (1984). *A Room of one's own* Penguin, Harmondsworth.

Wafula R.M (1999). *Uhakiki wa Tamthilia. Historia na Maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Kenya.

Wafula R.M na Kimani N. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi Kenya.

Wachira J.W (2006). 'Taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika nyimbo za kisasa za Rap.' Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Wamitila K.W (2002). *Uhakiki wa fasihi. Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers,Nairobi, Kenya

----------------- (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Focus Books Nairobi, Kenya.

---------------- (Mh) (2004) *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.* Focus Publishers, Nairobi, Kenya.

Wandera S.P (1996). 'Usawiri wa mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili 1800-1900. Uhalisi au ugandamizwaji?' Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta(Haijachapishwa).

Waweru,J (2006) 'Taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika nyimbo za kisasa za rap' .Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Z. Burhani (1981) *Mali ya Maskini.*E.A.P.H, Kenya.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY